OSORO G. MOGERE

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

FOR USE IN THE LIBRARY ONLY

UZAMILI WA SANAA (M.A)

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2003

EAST AFRICANA COLLECTION

# UHAKIKI WA RIWAYA ZA AHMED MOHAMED KATIKA MISINGI YA KIFEMINISTI

NA

OSORO G. MOGERE

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI WA SANAA.

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2003

University of NAIROBI Library
0370222 2

EAST AFRICANA COLLECTION

# YALIYOMO

UKURASA

Yaliyomo ........ (i) – (ii)

Ungamo ........ (iii)

Tabaruku ........ (iv)

Shukrani ........ (v)

Muhtasari ........ (vi)

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi ........ 1

1.1 Tatizo la utafiti ........ 4

1.2 Madhumuni ya tasnifu ........ 5

1.3 Nadharia tete ........ 5

1.4 Sababu za kuchagua mada ........ 6

1.5 Upeo na mipaka ya tasnifu ........ 6

1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada ........ 7

1.7 Msingi wa kinadharia ........ 10

1.8 Njia za utafiti ........ 14

Tanbihi ........ 15

SURA YA PILI : ASALI CHUNGU NA UTENGANO

2.0 Utangulizi ........ 16

2.1.1 Mhutasari wa Riwaya ya Asali Chungu ........ 18

2.1.2 Mhutasari wa Riwaya ya Utengano ........ 18

2.2 Mwanamke Kisheria ........ 19

2.3 Mwanamke Kielimu ........ 23

2.4 Mwanamke Kiuchumi ........ 27

2.5 Malezi ya mtoto wa kike ........ 30

2.6 Mwanamke katika ndoa ........ 32

2.7 Mwanamke Kisiasa ........ 36

2.8 Hitimisho ........ 41

Tanbihi ........ 42

SURA YA TATU : KIZA KATIKA NURU NA TATA ZA ASUMINI

3.0 Utangulizi .......................................................... 43
3.1.1 Muhtasari wa riwaya ya Kiza Katika Nuru ................ 43
3.1.2 Muhtasari wa Tata za Asumini .............................. 45
3.2 Mwanamke na utamaduni ....................................... 46
3.3 Mwanamke katika siasa ......................................... 52
3.4 Mwanamke Kielimu ................................................ 57
3.5 Mwanamke Kiuchumi ............................................. 58
3.6 Hitimisho ........................................................... 59
Tanbihi ................................................................. 60

SURA YA NNE : KUSAWIRIWA KWA WANAWAKE

4.0 Utangulizi .......................................................... 61
4.1 Mwanamke kama mdhulumiwa ................................ 62
4.1.1 Mwanamke kama mfanyakazi ................................ 63
4.1.2 Mwanamke katika ndoa ........................................ 66
4.1.3 Malezi ya mtoto wa kike ...................................... 68
4.2 Mwanamke kama kahaba ....................................... 69
4.3 Mwanamke kama mwanasiasa ................................ 70
4.4 Hitimisho ........................................................... 72
Tanbihi ................................................................. 73

SURA YA TANO

5.0 Hitimisho ........................................................... 74
5.1 Kufanikiwa na kutofanikiwa kwa mwandishi ................ 76
5.2 Kuhusu nadharia tete ............................................ 77
5.3 Mapendekezo kuhusu utafiti zaidi .............................. 78
Marejeleo .............................................................. 79 - 84

# UNGAMO

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya digrii katika chuo kikuu kingine chochote"

**OSORO G. MOGERE**
**(Mtahiniwa)**

"Tasnifu hii imeandikwa, kutolewa na kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa chuo kikuu."

**DKT. MWENDA MBATIAH**
**(Msimamizi)**

**NDG. BASILIO MUNGANIA**
**(Msimamizi)**

## TABARUKU

*Kwa ukumbusho na heshima ya marehemu babangu, Jeremiah Osoro.*

# SHUKRANI

Natoa shukrani kwa wasimamizi wangu katika kazi hii Dkt. Mwenda Mbatiah na Mw. Mungania Gichobi. Uongozi wao ulinifaa nilipokuwa nikiendelea na utafiti wangu.

Aidha nawashukuru wahadhiri wa Idara ya Isimu Lugha za Kiafrika hasa wale walionifunza darasani na kuhakikisha kukamilika kwa masomo yangu ya uzamili kwa wakati uliofaa. Wahadhiri hao ni pamoja na. Prof. Mohamed Abdulaziz.Mw. Timothy Arege. Dkt. Buregeya na Dkt. Mutiso wa Kineene na Mw. Richard Mgullu.

Nawashukuru pia Dkt. Kithaka wa Mberia ambaye ni mkuu wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika na Ndg. Mohammed Akida mratibu wa mipango ya uzamili katika idara. Pia siwezi kumsahau Dkt. Francis Eshun. Kwa juhudi zao. masomo yangu yaliweza kuendelea na kukamilika kwa wakati uliofaa.

Ningependa pia kuwataja wanafunzi wenzangu tulioshirikiana nao katika bahari hii ya usomi. Wao ni pamoja na: Bwire Tobias. Prisca Jerono. Grace Chiuri na Perminas Nzuki. Wanafunzi wengine ambao siwezi kuwasahau ni. Tola Kofa. Fred Magare na Vince Arasa Nyabunga.

Namshukuru mamangu Priscilla Kwamboka Osoro kwa kushirikiana na marehemu babangu Jeremiah Osoro katika kuhakikisha kwamba niliweza kusoma ingawa kwa kujifunga kibwebwe.

Naishukuru pia aila yangu. Bi. Beatrice Bochere Mogere. watoto. Boniface Omboga Mogere na Ezra Nyabuti Mogere kwa uvumilivu wao wakati nikijishugulisha na masomo ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Pia nawashukuru wafuatao waliochukua muda wao mwingi ili kuhakikisha kwamba kazi hii ilichapishwa kwa uangalifu mkubwa ingawa makosa hayakosekani jinsi wahenga walivyosema "hakuna kizuri kisicho na dosari." Wao ni pamoja na David Ogamba. Sarah Nyangena na wafanya kazi wote wa LEMMA Cyber Café.

Kwa wale wote niliowataja na wale sikuweza kuwataja. nawaombea kila la heri maishani mwenu.

# MUHTASARI

Tasnifu hii imeshughulikia uhakiki wa Riwaya za Said Ahmed Mohamed katika misingi ya kifeministi Riwaya tulizozitumia kama sampuli katika uhakiki huu ni nne nazo ni *Asali Chungu* (1977) *Utengano* (1980), *Kiza Katika Nuru* (1988) na *Tata za Asumini* (1990). Tasnifu hii ina sura tano.

Katika sura ya kwanza tumejadili, somo la utafiti, sababu za kulichagua na madhumuni. Maelezo kuhusu mipaka na upeo wa tasnifu pia yametolewa katika sura hii. Katika sura hii pia tumeyajadili yaliyoandikwa kuhusu mada na hatimaye tumeeleza matawi mbalimbali ya nadharia tuliyotumia.

Sura ya pili inahusu maudhui ya Kifeministi katika riwaya za *Asali Chungu* na *Utengano*. Tumetoa muhtasari wa riwaya hizi mbili, maudhui ya kisiasa, kielimu, kisheria, kiuchumi, malezi ya mtoto wa kike na pia mwanamke katika ndoa.

Sura ya tatu ni kama inaendelea kuyachunguza maudhui ya kifeministi lakini kwa kurejelea riwaya za *Kiza Katika Nuru* na *Tata za Asumini*. Mambo tuliyotazama ni pamoja na mwanamke na utamaduni, mwanamke kielimu mwanamke kisiasa na pia mwanamke kiuchumi.

Sura ya nne inashughulikia suala la usawiri wa wahusika wa kike katika riwaya za S.A Mohamed.

Sura ya tano ni hitimisho. Tumerejelea yale yote yaliyojadiliwa katika sura zote. Pia tumetoa maoni yetu na mapendekezo kuhusu kufanywa kwa utafuti zaidi.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Mada ya tasnifu hii ni *Uhakiki wa Riwaya za Said Ahmed Mohamed katika misingi ya Kifeministi.*

Uhakiki wa kifeministi unahusu uchunguzi wa kazi za sanaa kwa kuzingatia mtazamo wa kike. Tasnifu hii itajishughulisha na kuyachunguza matatizo yanayowakumba wanawake, chanzo cha matatizo hayo, harakati zao katika kujitafutia ukombozi kama yanavyojitokeza katika riwaya za Said Ahmed Mohamed. Kabla hatujajishughulisha na riwaya, ni vizuri kueleza maana ya ufeministi kwanza.

Tuttle, anaeleza kuwa, huko mwanzoni, ufeministi ulimaanisha hali ya kuwa na sifa za kike lakini baadaye istilahi hii ikaanza kutumiwa kurejelea upiganiaji wa haki za wanawake [1].

Usawiri wa wahusika wa kike katika fasihi ya Kiswahili ni suala lililo na utata mwingi kufikia sasa. Inadaiwa kwamba wanawake wanasawiriwa kwa njia isiyofaa hasa katika kazi zilizoandikwa na wanaume. Wanaodai hivi wanasema kwamba mwanamume anapoandika kazi ya kifasihi huwaonea wanawake na kuwasawiri wahusika wa kike kwa njia isiyopendeza huku akiwapendelea wahusika wa kiume. Wahakiki wengine hudai kwamba tamaduni huchangia pakubwa katika kusawiriwa kwa wahusika wa kike. Jambo hili linadhihirika wazi tunapousoma *Utenzi wa Mwanakupona* ambao ulibuniwa na

mwanamke. Mwanakupona anamuusia bintiye jinsi anavyoweza kuishi kwa kumridhisha mumewe. Mwanakupona hapendekezi vile mwanamume naye anaweza kumridhisha mwanamke. Mwanakupona anaongozwa na imani na tamaduni zinazomdunisha mwanamke. Uhakiki wetu utachunguza vile Said Ahmed Mohamed anavyolishughulikia suala hili katika riwaya zake.

Uhakiki wa aina hii uliibuka na kuwa maarufu kuanzia karne ya kumi na nane kufuatia mwamko wa wanawake katika kudai na kutetea haki zao.

Tangu kuchimbuka kwa tapo hili huko Ulaya, ufeministi umepitia katika vipindi viwili tofauti. Vipindi hivi ni pamoja na kile cha kwanza (1860-1920) na kikafuatiwa na kipindi cha pili kuanzia miaka ya 1960 hadi leo. Uhakiki mpya unahusishwa na kipindi cha pili.

Kipindi cha kwanza kinarejelea juhudi za wanawake wa awali katika kupigania haki zao. Mwandishi na mtetezi sugu wa haki za wanawake anayehusishwa na kipindi hiki ni Mary Wollstonecraft ambaye aliandika kitabu maarufu cha *A Vindication of the Rights of Women (1792).*

Kipindi cha pili kilichojitokeza kuanzia miaka ya 1960 hadi hivi sasa kinahusishwa na waandishi maarufu Virginia Woolf na Simone de Beauvoire.

Wafuasi wa ufeministi katika kipindi hiki wanatumia maandishi katika kushambulia asasi zilizopo katika jamii ambazo zinachangia udhalilishwaji wa wanawake. Asasi hizo ni pamoja na zile za kiuchumi na za kisiasa. Wanajishughulisha na kubuni mbinu mpya za kupigania ukombozi wa wanawake. Wanaharakati katika kipindi hiki wanatumia mbinu mbalimbali zikiwemo, kuandika makala, utafiti, ushairi, riwaya, sanaa za maonyesho na majarida ili kuwahamasisha wanawake waanze kupigania haki zao.

Kulingana na Davis na Schleifer (1989), uhakiki wa kifeministi katika kipindi hiki unahusishwa na kazi za waandishi wawili maarufu, Virginia Woolf na Simone de Beauvoire[2]. Hadi sasa kazi za waandishi hawa ni maarufu na muhimu sana katika uwanja wa uhakiki. Kazi za waandishi hawa ambazo ziliwapa umaarufu ni pamoja na *A Room of One's Own* (1928) *ya* Virginia Woolf na *The Second Sex* (1949*) ya* Simone de Beauvoire

Andrene Rich (1989) katika *Contemporary Literary Criticism*, anapendekeza kuwa uhakiki wa kifeministi unafaa uonyeshe jinsi tumekuwa tukiishi, jinsi tulivyoongozwa kujifikiria, jinsi lugha yetu imetufunga na vilevile kutukomboa, jinsi tunavyoweza kuona na kuanza kuishi upya[3]. Mwandishi huyu anatambua kuwa kupitia kwa uhakiki, tataona vile vile tumekuwa tukiishi,vile tunaishi, makosa tuliyoyafanya na kuyarekebisha ili tuanze kuishi kwa njia inayofaa.

Mbali na riwaya, Said Ahmed Mohamed amewahi kuandika mikusanyiko ya mashairi, hadithi fupi na Tamthilia pia ameandika kuhusu semi za Kiswahili.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Tatizo tunalolichunguza katika utafiti wetu ni kuzihakiki riwaya za Said Ahmed Mohamed katika misingi ya kifeministi. Suala kuhusu usawiri wa wahusika wa kike katika fasihi limekuwa likishughulikiwa kwa muda mrefu hasa kuanzia karne ya kumi na nane. Katika fasihi ya Kiswahili, suala hili limeanza kushughulikiwa hivi karibuni hasa baada ya ukoloni lakini bado lina utata mwingi. Kulingana na maoni yetu usawiri wa wahusika wa kike katika fasihi bado upo katika kiwango kisichoridhisha na unastahili kuchunguzwa zaidi.

Katika uhakiki wetu, tunatazamia kuchunguza jinsi suala hili limejitokeza katika riwaya za Said Ahmed Mohamed. Tutachunguza vile mwandishi alivyoyashughulikia matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii, kinachosababisha matatizo hayo, juhudi za mwanamke katika kujikomboa, na pia uhusiano uliopo baina ya wanawake na wanaume.

Baada ya kuona vile mwandishi alivyoshughulikia mambo hayo, basi nafasi yake katika uwasilishaji wa masuala kuhusu mwanamke itaweza kutambulikana.

## 1.2 MADHUMUNI YA TASNIFU

(i) Kuchunguza jinsi wahusika wa kike walivyosawiriwa katika riwaya za Said Ahmed Mohamed.

(ii) Kuweka wazi matatizo yanayowakumba wanawake jinsi yanavyojitokeza katika riwaya za Said Ahmed Mohamed.

(ii) Kuchunguza juhudi zinazofanywa na wanawake katika kutafuta ukombozi wao.

(iii) Kutathamini nafasi ya Said Ahmed Mohamed katika kuyashughulikia masuala yanayowahusu wanawake. Hapa tutaona ikiwa amewasawiri kwa njia nzuri au la.

## 1.3 NADHARIA TETE

(i) Katika riwaya za Said Ahmed Mohamed wahusika wa kike wamesawiriwa kwa njia mbalimbali.

(ii) Said Ahmed Mohamed ameyaangazia matatizo yanayowakumba wanawake katika jamii huku akionyesha chanzo cha matatizo hayo.

(iii) Mwandishi ametambua juhudi mbalimbali zinazofanywa na wanawake katika kutafuta ukombozi wao na ule wa jamii kwa jumla.

## 1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Usawiri wa wahusika wa kike katika fasihi ya Kiswahili ni suala lililo na utata mwingi na bado halijashughulikiwa ipasavyo.Utata ulioko ni kwamba kuna madai kuwa wahusika wa kike hawasawiriwi kwa njia nzuri. Kwa hivyo sababu za kuchagua mada hii ni pamoja na:-

(i) Kuuongezea tahakiki kuhusu kusawiriwa kwa wanawake.

(ii) Kwa sasa kuna harakati zinazoendelea za kupigania ukombozi haki na usawa wa wanawake katika jamii. Katika kushughulikia mada hii, tutakuwa tunatoa mchango wetu katika harakati za kumkomboa mwanamke kama anavyosema Ndungo (1985) kwamba ukombozi wa wanawake hauwezi kupatikana bila jamii nzima, wanawake kwa wanaume kushiriki[4].

## 1.5 UPEO NA MIPAKA YA TASNIFU

Tasnifu yetu itajikita katika uchunguzi wa maudhui ya kifeministi na usawiri wa wanawake, katika riwaya za Said Ahmed Mohamed. Kazi ambazo tutazizingatia katika uhakiki wetu ni pamoja na, *Asali Chungu* (1977), *Utengano* (1980), *Kiza Katika Nuru* (1988) *na Tata za Asumini* (1990).

Tuliziteua kazi hizi kama sampuli kwa sababu ya muda mfupi ambao hungeturuhusu kuzishughulikia riwaya zote za mwandishi huyu. Tulitumia njia ya bahati nasibu ambapo

kila moja kati ya riwaya za Said Ahmed Mohamed ilikuwa katika nafasi ya kuweza kuteuliwa. Hata hivyo uteuzi huu haumaanishi kwamba hizi ndizo tu riwaya za Said Ahmed Mohamed zinazoyashughulikia maudhui ya kifeministi.

Sababu ya kuziteua kazi hizi nne ni wakati mfupi tuliokuwa nao. Muda mfupi tuliokuwa nao haungeturuhusu kuzishughulikia riwaya zote za mwandishi tunayemhakiki.

Katika kufanya uteuzi huu, tumejaribu kujiepusha na kuyarudiarudia baadhi ya maudhui.

Baada ya kufanya uteuzi wetu, tumeamua kuzishughulikia riwaya hizi katika makundi mawili kwa kuzingatia kipengele cha wakati zilipoandikwa. Tumeamua kushughulikia *Asali Chungu* (1977) na *Utengano* (1980) kama kundi moja na pia *Kiza Katika Nuru* (1988) *na Tata za Asumini* (1990) kama kundi moja. Temeamua kuzigawa jinsi hii kwa vile baadhi ya maudhui katika riwaya hizi huenda yakafanana kwa sababu ya upana wa kiwakati. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunajiepusha na kurudiarudia baadhi ya maudhui.

## 1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Kufikia sasa, mengi yameandikwa kuhusu masuala ya wanawake. Wahakiki wengi wameshughulikia maudhui katika riwaya za Said Ahmed Mohamed kwa viwango mbalimbali.

Mbughuni, P (1982) *Usawiri wa Wanawake katika Riwaya za Kiswahili*, anadai kwamba wanawake wengi wamesawiriwa kama makahaba na kubainisha kuwa kuwepo kwa wahusika wengi makahaba katika riwaya za Tanzania hakumaanishi kwamba nchi hii ina idadi kubwa ya makahaba. Kazi hii ya mbughuni ni muhimu kwa vile itachangia katika kutambua chanzo cha matatizo ya wanawake na kwa nini wengi wao huamua kuingilia mambo ya ufasiki.

Kamunde,S (1983) *Kilio Cha Wanyonge katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed*, ameshughulikia matatizo yanayowakumba wanyonge wanaume kwa wanawake jinsi yanavyojitokeza katika riwaya za Said Ahmed Mohamed.

Kazi hii itatusaidia kutambua jinsi mwanamke na mwanamume wanavyosawiriwa kama kundi linalodhulumiwa.

Ndungo, C (1985) *Usawiri wa Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili*, amemtazama mwanamke jinsi anavyosawiriwa katika vipindi mbali mbali vya kihistoria. Pia kazi hii ni muhimu kwa vile imeangazia vile wanawake wamekua wakisawiriwa kwa njia isiyofaa.

Lugano, R (1989) *Usawiri wa Wanawake katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi* amechunguza jinsi Kezilahabi anavyowasawiri wahusika wa kike katika nyanja mbali mbali za maisha. Pia ameyashughulikia maoni ya Kezilahabi mwenyewe kumhusu mwanamke katika nyanja za siasa, uchumi, jamii na elimu. Kazi hii ya Lughano ni

muhimu kwetu hasa kwa kutudokezea jumla ya matatizo yanayowakumba wanawake katika jamii jambo ambalo ni la kimsingi katika utafiti wetu.

Muindi, J (1990) *Usawiri wa wahusika makahaba katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed*, amechunguza jinsi wanawake walivyosawiriwa kama makahaba na kutoa sababu zake. Kwa vile wanawake wengi huingilia ukahaba kwa sababu ya matatizo mbali mbali ya kijamii ambayo uhakiki wetu unajishughulisha nayo, kazi ya Muindi itakuwa muhimu kwetu kwa kutudokezea kinachosababisha wanawake kuingilia kitendo cha ukahaba.

Njogu, K (1997) *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*, amegusia matatizo yanayowakumba wanawake katika jamii. Ingawa katika kazi hii mwandishi hajalipa suala la kifeministi nafasi kubwa, aliyoyazungumzia kumhusu mwanamke akidhulumiwa katika jamii yatatusaidia katika ujenzi wa maudhui yetu.

Nyamberi, H (1997) *Mwamko wa wanawake katika Tamthilia Nne za Penina Muhando*, anachunguza jinsi mwanamke ameanza kuhisi akidhulumiwa na hivyo kuanza kudai haki zake. Ingawa Nyamberi anajishughulisha na kuzihakiki tamthilia, baadhi ya maudhui yake kama vile chanzo cha mwamko wa wanawake ni muhimu kwa utafiti huu.

Momanyi, C (2002) *Suala la Uana katika utafiti wa Fasihi*, amejikita kwenye nadharia. Kwa vile nadharia ndio nguzo muhimu katika kazi za kihakiki hususani kazi yetu, kazi ya

Momanyi itatufaa katika kutambua jinsi ya kuoanisha nadharia na kazi tunayoishughulikia.

Khaemba, S (1999) *Ulinganishi wa maudhui ya mapinduzi katika Dunia Mti Mkavu (1980) na Kiza Katika Nuru* (1988), ameshughulikia mapinduzi dhidi ya tawala dhalimu kwa jumla. Kazi ya Khaemba ni muhimu kwa vile inaangazia mapinduzi ambayo wanawake pia ni washiriki. Itachangia kutambua nafasi ya mwanamke katika harakati za ukombozi.

## 1.7 MSINGI WA KINADHARIA

Nadharia itakayoongoza uchunguzi wetu ni ile ya kifeministi. TUKI (1986) wanaeleza kwamba ufeministi ni nadharia ya usawa wa wanawake[5]. Wanachomaanisha hapa ni kwamba hii ni nadharia inayopendekeza kupiganiwa kwa ukombozi, haki na usawa kati ya wanawake na wanaume.

Nadharia ya kifeministi iliasisiwa kutokana na kuzuka kwa tapo la ufeministi huko Ulaya. Wafuasi wa nadharia hii kama anavyosema Mbatiah (2001), wanachukua mwelekeo wa kiharakati na kushambulia baadhi ya asasi zinazochangia katika kumdhalilisha mwanamke [6].

Msingi wa nadharia hii unapatikana katika kazi ya Mary Wollstonecraft, *A Vindication of the Rights of Women* (1792) ambapo anapendekeza kuundwa kwa jamii mpya yenye usawa kati ya wanawake na wanaume. Wollstonecraft ni miongoni mwa waandishi wa

awali ambao pia walikuwa watetezi sugu wa haki za wanawake. Kazi zingine za awali ambazo ziliipa nadharia hii nguvu za kimsingi ni pamoja na *A Room of One's Own* (1929) ya Virginia Woolf na *The Second Sex* (1949) ya Simone de Beauvoire. Kulingana na Wollstonecraft, elimu ndicho kitu cha msingi katika harakati za ukombozi wa wanawake.

Anapendekeza kwamba wasichana wapewe elimu sawa na wavulana. Wollstonecraft anashauri kwamba wasichana wakipata elimu, watakuwa katika nafasi bora katika kupigania haki zao.

Woolf naye analisisitizia wazo hili huku akiongezea kwamba ni muhimu kwa mwanamke kuwa huru kiuchumi. Kulingana na Woolf, mwanamke akiwa na elimu na pesa, atajitegemea na kufanikiwa katika taaluma ya uandishi.

Nadharia ya kifeministi inapinga asasi zozote katika jamii ambazo zinachangia katika kumdhulumu mwanamke. Wafuasi wa nadharia hii wanapendekeza kuwe na usawa kati ya wanawake na wanaume bila kuzingatia tofauti zao za kimaumbile.

Wasisi na wafuasi wa nadharia hii wanadai kwamba tamaduni nyingi katika jamii humpendelea mwanamume huku mwanamke akichukuliwa kama kiumbe duni na kwa hivyo wanapendekeza kwamba wanawake wajitokeze na kupigania uhuru wao dhidi ya wanaume.

Tangu nadharia hii iasisiwe, matawi mengi yamechipuka. Kila moja kati ya matawi hayo linapendekeza kinachopaswa kuzingatiwa katika uhakiki na pia katika harakati za kupigania haki na ukombozi wa wanawake. Kila tawi lina msimamo fulani maalum na pia wafuasi wake.

Tawi litakaloongoza tasnifu hii ni lile linalojulikana kama ufeministi huru. Miongoni Mwa matawi yote ya ufeministi,hili ndilo linalojulikana zaidi.Linao wafuasi wengi kuliko matawi mengine yote.

Ufeministi huru unajihusisha na kupigania haki na mabadiliko ya jumla katika jamii. Linapigania kumalizika kwa ubaguzi kati ya wanawake na wanaume. Wafuasi wa tawi hili wanapendekeza kutekelezwa kwa mabadiliko kupitia kwa njia kama vile; ushawishi,mwamko wa kitabaka kushitaki na pia kupigania kujumuishwa kwa masuala yanayowahusu wanawake katika kila eneo la kimaisha. Tuttle (1986) anasema kwamba mwanafalsafa wa kwanza wa ufeministi huru ni Mary Wollstonecraft ambaye ni muasisi wa ufeministi kwa jumla.

Tawi hili linakubali ukweli kwamba mwanamke na mwanamume lazima washirikiane katika nyanja mbalimbali maishani.Kinachohitajika ni kubadilishwa kwa mtazamo wa jamii ili mwanamke aweze kutambuliwa kama binadamu sawa na mwanamume.

Uhakiki wa kifeministi una malengo mbalimbali.Yafuatayo ni baadhi ya malengo ya uhakiki wa aina hii.

(i) Kupigania kubuniwa kwa utamaduni wa kike. Hapa uhakiki unatumiwa kupinga tamaduni zinazompendelea mwanamume katika kutafuta kuundwa kwa utamaduni unaowatambua wanawake.

(ii) Kuweka wazi na kufasiri mawazo yanayojitokeza katika kazi zilizotungwa na wanawake ili zisionekane kuwa duni zinapopimwa kwa mizani ya kiume.

(iii) Kufumbua upya kazi za awali zilizoandikwa na wanawake. Kuna kazi nyingi zilizoandikwa na wanawake lakini zikapuuzwa kwa sababu ya kudharauliwa kwa wanawake. Kazi za aina hii ndizo ufeministi unapigania zishughulikiwe katika uakiki ili nafasi ya waandishi wa kike wa awali itambuliwe.

(iv) Kuziangalia upya kazi zilizoandikwa na wanaume kwa mtazamo wa kike kama asemavyo Maggie(1986) kwamba uhakiki wa kifeministi ni uchunguzi kuhusu usawiri wa kijinsia na itikadi katika fasihi kwa mtazamo wa kike.[8]

(v) Kuchunguza jinsi lugha inavyotumiwa kuashiria mambo mbalimbali katika fasihi. Lugha ya kifasihi hutumika kusawiri mambo mbalimbali kuliko jinsi lugha hiyo hiyo inaweza kutumika katika muktadha usio wa kifasihi.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti wetu umejikita kwenye maktaba. Umehusu kusoma kazi mbalimbali za Said Ahmed Mohamed hasa zile za Riwaya.

Pia tulisoma kazi mbalimbali kuhusu nadharia na ufeministi kwa jumla zikiwemo makala, majarida, tasnifu mbalimbali na kazi zingine nyingi zilizokuwa za manufaa kwa utafiti huu. Tumeshirikiana pia na wataalam mbalimbali ambao wamechangia pakubwa katika kufanikisha mradi huu.

## TANBIHI


1. Tuttle, L (1986), *Encyclopedia of Feminism* UK 105.
2. Davis, R, Schleifer, R (1989), *Contemporary Criticism* UK 450
3. Kama 2 UK 659
4. Ndungu, M (1985) *Tasnifu ya Uzamili* UK 147
5. Tuki (1996) English –*Kiwahili Dictionary* UK 278
6. Mbatiah, M (2001) *Kamusi ya Fasihi* UK 87
7. Fokkema, D.W, Kunne–Ibsch, E (1978) *Theories of literature in the Twentient Century* UK 86.
8. Maggie, H (1986) *Feminist Literary Criticism in America and England* in WOMEN'S WRITING: A Challenge to Theory UK 90

## TANBIHI

1. Tuttle, L (1986), *Encyclopedia of Feminism* UK 105.
2. Davis, R, Schleifer, R (1989), *Contemporary Criticism* UK 450
3. Kama 2 UK 659
4. Ndungu, M (1985) *Tasnifu ya Uzamili* UK 147
5. Tuki (1996) English –*Kiwahili Dictionary* UK 278
6. Mbatiah, M (2001) *Kamusi ya Fasihi* UK 87
7. Fokkema, D.W, Kunne–Ibsch, E (1978) *Theories of literature in the Twentient Century* UK 86.
8. Maggie, H (1986) *Feminist Literary Criticism in America and England* in WOMEN'S WRITING: A Challenge to Theory UK 90

## TANBIHI

1. Tuttle, L (1986), *Encyclopedia of Feminism* UK 105.
2. Davis, R, Schleifer, R (1989), *Contemporary Criticism* UK 450
3. Kama 2 UK 659
4. Ndungu, M (1985) *Tasnifu ya Uzamili* UK 147
5. Tuki (1996) English –*Kiwahili Dictionary* UK 278
6. Mbatiah, M (2001) *Kamusi ya Fasihi* UK 87
7. Fokkema, D.W, Kunne–Ibsch, E (1978) *Theories of literature in the Twentient Century* UK 86.
8. Maggie, H (1986) *Feminist Literary Criticism in America and England* in WOMEN'S WRITING: A Challenge to Theory UK 90

# SURA YA PILI

## *ASALI CHUNGU NA UTENGANO*

### 2.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tunachunguza kujadili maudhui ya kifeministi jinsi yanavyojitokeza katika riwaya za *Asali Chungu* (1977) na *Utengano* (1980). Riwaya hizi ni miongoni mwa kazi za kwanza kabisa za Said Ahmed Mohamed kuwahi kuchapishwa huku *Asali chungu* ikiwa ya kwanza kabisa.

Virginia Woolf, anapendekeza kwamba uhakiki wa kifeministi unapaswa kuyachunguza masuala ya kiuchumi, kisiasa na kijamii ambayo huchangia pakubwa katika udhalilishwaji wa mwanamke. Kulingana na Woolf, miongoni mwa masuala ambayo huchangia katika unyanyaswaji wa mwanamke ni pamoja na ndoa, mila, dini kunyimwa nafasi za elimu na mifumo ya kisheria.

*Asali Chungu* na *Utengano* ni riwaya za kijamii zinazoyamulika maisha ya waafrika katika vipindi viwili tofauti. *Asali Chungu* inaangazia maisha ya Wafrika wakati wa ukoloni huku *Utengano* ikiyamulika maisha katika jamii iliyo huru. Uchunguzi wetu utajikita katika kuchunguza jinsi mwanamke amesawiriwa katika riwaya hizi. Tunachunguza jinsi mwandishi ameyaangazia maisha ya wanawake, madhila

wanayopitia na pia juhudi mbalimbali wanazozifanya katika kuimarisha hali yao ya maisha katika maneno ya kiuchumi, kisiasa na pia kijamii.

### *2.1.1 MUHTASARI WA RIWAYA YA ASALI CHUNGU*

Riwaya ya *Asali Chungu* ni miongoni mwa kazi za sanaa kutoka Visiwani Zanzibar ambazo zinayamulika maisha ya jamii katika kipindi cha utawala wa kikoloni. Mwandishi ameitumia migogoro katika aila ya Bwana Zuberi kuwakilisha hali ya maisha katika jamii kwa wakati huo.

Bwana Zuberi ni DC katika utawala wa kikoloni naye Amina ni mkewe aliye na uwezo kiuchumi. Ana pesa anazozitumia kuwateka vijana barubaru.

Bwana Zuberi anawanyanyasa wananchi kwa njia mbalimbali. Anaowadhulumu zaidi ni wanawake. Anawateka wasichana warembo na kuwalazimisha kushiriki naye kimapenzi. Bwana Zuberi anamnajisi Semeni ambaye ni mtumishi wake kitendo ambacho kinayaharibu maisha yake. Baada ya kunajisiwa Semeni anaingilia mambo ya ukahaba.

Bi Amina kwa upande wake naye hatoshelezwi kimapenzi na mumewe Bwana Zuberi. Anawanasa vijana wadogo kama vile Dude ambao anawatumia katika kuzima uchu wake. Katika njama zake anawatumia Bushiri na Biti Daudi ambaye pia Bwana Zuberi anamtumia kwa njama kama hizi. Amina anatamani mumewe afe ili waweze kuishi na

Dude kama mume na mke. Baada ya Dude kukosana na Amina na kuhama, anarudi baadaye na Shemsha bintiye Amina kama mchumba wake na hatimaye wanaoana.

Muda mfupi kabla Bi Pili hajafariki, anamdokezea Dude kwamba Bwana Zuberi ndiye babake. Dude alizaliwa baada ya kile kitendo cha Bwana Zuberi cha kumnajisi Semeni. Dude amejua jambo hili baada ya kushirikiana kimapenzi na Amina ambaye ni kama mamake wa kambo, Shemsa na Laitifa ambao ni dada zake.

Baada ya kifo cha Zuberi na Amina, Dude, Shemsa na Laitifa wanashikana mikono. Kifo cha Amina na Zuberi na mlipuko unaotoka ni ishara ya mapinduzi ya mwaka wa 1964 kule visiwani Zanzibar.

### 2.1.2 *MUHTASARI WA RIWAYA YA UTENGANO*

Jamaa ya Maksuudi inawakilisha migogoro katika jamii baada ya kutimuliwa kwa utawala wa kikoloni. Maksuudi ni Shekhe na Bi Tamima ni mkewe, Mussa ni mwanao wa kiume na Maimuna mwanao wa kike.

Bwana Maksuudi anamwendea kinyume mkewe kwa kushiriki mapenzi na wanawake wengine. Kitendo hiki kinampeleka pale kwa Kazija ambapo anamfumania mwanaye Mussa. Bi Tamima na Maimuna bintiye hawaruhusiwi na Bwana Maksuudi kutoka nyumbani jambo ambalo Maimuna analichukia.

Biti Kocho amejitolea kupinga vitendo vyake Maksuudi. Biti Kocho anampinga Maksuudi pale anapompiga Bi Tamima akiwa kwenye maumivu baada ya uzazi. Biti Kocho anapinga pia kitendo cha Bwana Maksuudi kutowaruhusu Bi Tamima na Maimuna kutoka nje kama wanawake wengine.

Biti Kocho na Farashuu wanapanga njama na kumtorosha Maimuna kutoka kwao. Pia Bi Tamima naye anahama kwake baada ya kudhulumiwa kwa kupigwa na Bwana Maksuudi. Kutoroka kwa Maimuna akiutafuta uhuru kunampeleka kuingilia maisha ya ukahaba.

Kazija, anauchochea umma dhidi ya Maksuudi katika uwanja wa uhuru kitendo ambacho hatimaye kinapelekea kukamatwa na kufungwa kwa Maksuudi kifungo cha miaka miwili gerezani. Kazija anaugeuza mtazamo wa wananchi kisiasa na kuelekeza mkondo wa uchaguzi kwa kuangazi maovu ya wagombeaji kura kama vile Maksuudi na Zenga.

Mwisho Maimuna amesawiriwa akiacha maisha ya ukahaba na kuolewa na Kabi kijana ambaye ni mwanaye Maksuudi na Bi Mwanasururu aliyetalikiana naye na mwishowe akafa.

## 2.2 MWANAMKE KISHERIA

Mary WollStonecraft, analilia usawa katika utekelezaji wa sheria pamoja na masuala mengine yote katika jamii. Anapendekeza wanawake watazamwe kama viumbe walio na haki sawa na wanaume. Katika *Asali Chungu* na *Utengano*

Said Ahmed Mohamed ameonyesha jinsi kuna ukosefu wa haki wakati wa kutekelezwa kwa sheria na anayelemewa ni mwanamke.

Katika riwaya ya *Asali Chungu*, ni siku ya wanawake na wanaonekana wakiketi nje ya ofisi ya DC. Wanawake hawa wanatarajia kuona haki ikitekelezwa ili wamwone Bwana DC. lakini wapi? Haki haitekelezwi. Bwana DC anatumia muda wake mwingi kuwahudumia wasichana warembo ambao anawanyanyasa kimapenzi.

Vitendo vya aina hii ni vya kidhalimu ambavyo vinakiuka haki za kibinadamu. Wanawake wanataka kulalamikia dhuluma kutoka kwa wafanyakazi wa Bwana DC. Hata hivyo Bwana DC ana wapuuza wanawake hawa na kuwatumikia warembo walio tayari kuutukana uke wao ili waweza kupata nafasi ya kuwatumikia.

Mhusika Semeni katika riwaya ya *Asali Chungu* ni mtumishi wa Bwana DC. Bwana Zuberi anatamani kufanya mapenzi na Semeni, lakini anashindwa kumshawishi. Semeni haogopi kuwa Zuberi ni mwajiri wake. Kile anachokithamini ni heshima yake. Hataki kuvunjiwa heshima yake kwa kushiriki kitendo kisicho halali. Binti Daudi ndiye wanayeshirikiana na Bwana Zuberi katika kupanga njama ya kumnajisi Semeni. Baada ya kushindwa kushawishi Semeni kufanya kitendo asichotaka, Zuberi anamnyemelea usiku akiwa usingizini, kumnyunyuzia Semeni dawa ya kulevya na hatimaye kumnajisi. Kitendo hiki kinasababisha kuzaliwa kwa Dude.

Baada ya kunajisiwa, Semeni anapahama pale kwa Bwana Zuberi na kumalizia kufanya ukahaba. Dhuluma kama hizi zinasababishwa na kutokuwepo kwa sheria maalum ambazo zinalinda haki za binadamu hasa mwanamke. Semeni kama binadamu mwingine ana haki ya kufanya kazi kwenye mazingira yenye haki na uhuru. Dhuluma kama hii ya Zuberi kwa Semeni inatokana na ukosefu wa sheria za kulinda na kutetea maslahi ya wanawake hasa wanawake wafanya kazi. Wanawake wapiganie kuundwa kwa sheria za aina hii.

Tunapoangalia riwaya ya *Utengano*, mhusika Bi. Tamima anadhulumiwa kwa kunyimwa haki hata ya kuyatawala maisha yake mwenyewe. Huku akiwa katika hali ya maumimvu ya uzazi, Bi. Tamima anaogopa hata kutafuta usaidizi wa daktari au mkunga yeyote. Anaogopa kwamba Bwana Zuberi atampiga akitafuta huduma kama hizi bila idhini yake. Hapa jamii imemfanya mwanamke aamini kwamba aliye na uwezo juu ya kila kitu hata kuyahusu maisha ya mwanamke ni mwanamume.

Dhuluma dhidi ya Semeni na pia Bi. Tamima zinaendelezwa kwa sababu ya ukosefu wa sheria za kushughulikia masuala kama haya na kama zipo basi hazitekelezwi. Wako wanawake wengi wanaopitia matatizo kama ya Semeni na Bi. Tamima katika jamii inayozungumziwa katika riwaya. Wanawake wengi wanaofanya kazi, iwe ya umma au ya kibinafsi chini ya usimamizi wa wanaume wanadhulumiwa bila kuwa na sheria ya kukimbilia.

Mapendekezo yetu kuhusu suala hili ni kwamba wanawake wapiganie kubuniwa kwa sheria ambazo zitawakinga kutokana na dhuluma mbalimbali maishani. Sheria kama hizi zikibuniwa, wanawake watakuwa na kimbilio badala ya kukimya au kujiingiza kwenye vitendo visivyofaa. Wanawake hawatanyanyaswa na kuungalia kwa ndani.

Pia tunawashauri wanawake washirikiane katika kutetea haki za wanawake wenzao kila mara wanapodhulumiwa. Mfano mzuri wa jinsi wanawake wanapaswa kushiriki katika harakati za kupigania ukombozi wa wanawake wenzao ni Bi. Pili katika riwaya ya *Asali Chungu*. Baada ya kugundua juu ya kitendo ambacho Bwana Zuberi alimfanyia Semeni, Pili anajitolea na kumkabili Bwana Zuberi katika Riwaya ya *Asali Chungu* ambapo anamwambia;

> Mimi nimekuja hapa kwa shauri la Semeni...niambie moja tu; umemweka wapi mpaka sasa? Usidhani yalikwisha baada ya kunifukuza siku ile nilipokuja kukushtakia hali yake. Nimeona sitakoma nije tena kukupa nafasi nyingine ya mwisho ya kuchagua kuficha aibu yako. Ukitaka ni kheri yako na kheri ya Semeni....[1]

Hatua ya Pili ni ya kijasiri ambayo inafaa kuigwa na wanawake katika kupigania haki zao. Pili hamuogopi Bwana DC kwa vile yeye anaona kwamba Bwana DC ni binadamu sawa na Semeni. Mwandishi amemsawiri mhusuka huyu ili awe kama kichocheo kwa wanawake ili wasinyamaze huku wakidhulumiwa.

Mpinzani mwingine ambaye ni mfano mzuri unaopaswa kuigwa na wanawake ni ule wa Biti Kocho katika Riwaya ya *Utengano*. Biti Kocho amejitolea katika kutetea haki za wanawake wenzake. Kupitia kwa Bi Tamina tunaona jinsi Bi Kocho anavyomkabili mwajiri wake Bwana Maksuudi ili akome kumdhulumu huyo bibi. Ingawa Biti Kocho ni mtumishi wa Bwana Maksuudi, hasiti kumwambia ukweli. Hata kama ni kuachishwa kazi Biti kocho hamuogopi. Anamzuia Maksuudi asiendelee kumpiga Bi Tamima. Biti Kocho anamwambia Bwana Maksuudi;

> Mabwana zaidi kuliko wewe sisi tuliwaondoa na penye haki sioni uzito wakukuita jina lolote. Naujue kuwa wakati utafika wanawake kuonekana watu, ala! [2]

Biti Kocho na Pili ni mifano mizuri ya wanawake wanaojitolea kwa vitendo katika kuyatetea masilahi ya wanawake wenzao katika jamii. Ni mifano ya kuigwa na wanawake wengine ili waungane na kushiriki katika kubuni mazingira yenye haki na usawa baina yao na waume. Kwanza wanawake watambue haki zao na pili watambue wamtambue adui anayewanyima haki hizi ili waweze kumkabili. Wanawake washiriki katika kuelimishana kuhusu haki zao ili panapotokea uhitaji wajue jinsi ya kutafuta usaidizi wa kisheria.

## 2.3 MWANAMKE KIELIMU

Katika jamii anayoindikia mwandishi, elimu kwa mtoto wa kike bado iko katika kiwango cha chini sana. Watoto wa kike hajapewa nafasi ya kusoma ikilinganishwa na watoto wa kiume. Kuna upendeleo katika kusambaza nafasi za elimu miongoni mwa watoto.

Katika kitabu chake *A vindication of the Rights of Women* (1792) Mary Wallstonecraft anadai kwamba unyonge wa mwanamke husababishwa na mfumo wa kijamii na hali hii inaweza kurekebishwa kwa kusambaza kiwango sawa cha elimu kwa watoto wote wasichana kwa wavulana. Kulingana na Wollstonecraft, baada ya wasichana kupokea elimu bora watakuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kupigania haki zao na pia kugombea nafasi mbalimbali katika jamii ambazo kwa sasa zinatwaliwa na wanaume.

Ukosefu wa elimu bora miongoni mwa wanawake wengi umesababisha hali ya kutojielewa kwao na hata pia kujua malengo yao. Elimu ni silaha muhimu katika maisha ya binadamu. Mwanamke akipokea elimu bora, anaweza kuwa katika nafasi nzuri ya kujikomboa. Matatizo mengi yanayowakabili wanawake yanatokana na kutojielewa na pia kutoelewa chanzo cha matatizo yao.

Katika riwaya za Said Ahmed Mohamed, suala la ukosefu wa elimu miongoni mwa wanawake limepewa nafasi kubwa. Madhila yanayowakumba wahusika wengi wa kike katika riwaya hii yanasababishwa na ukosefu wa elimu. Katika riwaya ya *Utengano,* Kazija anamlalamikia Mussa kuhusu jinsi wanawake walivyonyimwa nafasi za elimu huku wanaume wakinufaika:

> Nyinyi mliosoma elimu yenu bure. Hamjui mnakotoka wala
>
> mnakokwenda....kh, usinisemee kisungu miye. Si ndivyo
>
> mlivyotuweka? tusisome tuwe wajinga .Mtutawale na
>
> kutuparamia maisha, ao sivyo? [3]

Kazija ametambua kwamba ukosefu wa nafasi za elimu kwa upande wa wanawake kumesababishwa na mfumo wa kijamii unaotawaliwa na taasubi ya kiume. Wanaume wanapewa nafasi za kusoma huku wanawake wakinyimwa nafasi kama hizo. Mwandishi ametuonyesha hali kama hii kupitia kwa wahusika Mussa na Maimuna. Musa anapelekwa shuleni huku Maimuna akifungwa nyumbani pamoja na mamake. Hali hii inaonyesha jinsi wavulana wanavyopendelewa katika jamii na wasichana kupuuzwa. Wavulana wanapewa nafasi ya kusoma huku wasichana wakikaa kizuzu bila kujielewa wala kuelewa jamii.

Kwa sababu ya kukosa elimu, Maimuna haielewi jamii ndiyo maana anapoamua kutoroka kwao anatumbukia kwenye shimo la ukahaba. Kama Maimuna angekuwa na elimu, labda elimu hii ingemsaidia ajielewe na labda kuchagua maisha mema kuliko kuingilia mambo ya ukahaba. Mwandishi pia amedhihirisha kwamba msichana anaposomeshwa huwa ni kwa bahati tu.

Tunapomchunguza mhusika Shemsa wa riwaya ya *Asali Chungu*, yeye ni msomi na hata anafanya kazi ya udaktari. Yeye amepata nafasi hii ya kusoma kwa vile wazazi wake hawana mtoto wa kiume vile Bwana Zuberi anavyosema;

> Wewe unajua mke wangu unaelewa jinsi nilivyo kuwa nikitmani kupata mtoto wa kiume lakini wapi. Haidhuru. Mungu akatukosesha upande mmoja akatupa upande mwingine [4].

Kwa sababu Bwana Zuberi kakosa mtoto wa kiume, Shemsa anapata nafasi hii kibahati kama vile tulivyosema hapo mwanzo. Mbali na Shemsa wanawake wengine waliosawiriwa katika riwaya hizi mbili hawakusoma. Kulingana na Wollstonecraft, elimu ndiyo msingi wa kila kitu maishani na kuikosa ni kukosa kitu cha thamani kubwa sana katika maisha. Elimu ndiyo inaweza kumfanya mtu ajielewe, aielewe jamii na hata kupata kazi nzuri. Kuwanyima wasichana nafasi za elimu ni sawa na kuwalemaza maishani. Kazija katika *Utengano* analalamika;

> Mwanamume...elimu bora kwa mwanamume, haki zote kwa mwanamume, mwanamke nani mbele ya mwanamume? Ni pambo lilioko ndani, pambo la mwanamume ambalo alitazama, apumbae nalo. Alishika, ali.. Nani? Mwanamke, mtumwa. Nani kasema utumwa umeondoka? Viumbe vya kupika na kupakua, kufua na kupiga pasi, kushika mimba na kuzaa, kuzaa, kuzaa, kuzaa kama panya na kutawa na kutawishwa.[5]

Kazija anaeleza kwa uchungu kuhusu kazi ambazo mwanamke ametengewa kufanya katika jamii. Kulingana na Kazija, haya yote yanasababishwa na kutopewa elimu kwa wanawake. Wanawake wengi wanaosawiriwa katika riwaya hii wanafanya kazi duni kama vile kufanyia matajiri kazi za nyumbani. Kwa mfano watumishi wengi wanaotumikia Bwana Zuberi na Bwana Maksuudi majumbani mwao ni wanawake kulingana na Wollstonecraft, kukosa elimu ni sawa na kukosa kila kitu.

## 2.4 MWANAMKE KIUCHUMI

Virginia Woolf katika kitabu chake *A Room of One's Own* (1928), analipa uzito suala la uchumi katika ukombozi wa mwanamke. Kulingana na Woolf, mwanamke hawezi kupata ukombozi wa aina yoyote kama hajakombolewa kiuchumi.

Maisha ya binadamu mwanamke au mwanamume yanategemea hali ya uchumi. Hali ya uchumi ikiwa mbaya, maisha nayo yanakuwa mabaya. Wanaojiweza kiuchumi mara nyingi hutumia nguvu zao za kiuchumi kuwatawala na kuwanyanyasa wale ambao hawajiwezi kiuchumi. Wanawake ndio wanaathiriwa sana kwa vile wao wamenyimwa nafasi ya kujikuza kiuchumi. Nyenzo zote za kuzalisha mali zinatwaliwa na wanaume huku wanawake wakiwa wategemezi na watumishi wa wanaume. Wanawake wengi tunaokumbana nao katika riwaya hizi hawajakombolewa kiuchumi kwa vile wengi wao wanawategemea wanaume.

Semeni katika *Asali Chungu* anapoamua kutoroka kwa Zuberi baada ya kunajisiwa, anaingilia ukahaba kwa vile hana njia nyingine ya kuweza kujituma. Hapa ukosefu wa uhuru kiuchumi kunampeleka Semeni kwenye mitego ya wanaume walio na uwezo. Hapa Semeni hawezi kujitenga na wanaume ambao ndio chanzo cha matatizo yake. Semeni ametoroka Zuberi kwa sababu ya kudhulumiwa na uhitaji bado unamshurutisha kuwafurahisha wanaume huku akiutumia mwili wake.

Wafuasi wa ufeministi wanawahimiza wanawake watafute njia za kuwawezesha wajitegemee kiuchumi. Mbinu wanazozipendekeza ni pamoja na: kujiunga katika vikundi mbalimbali vya akina mama ili waweze kusaidiana na kupeana nguvu kiuchumi.

Katika *Asali Chungu* Bi Amina mwenyewe anakiri kwamba Bwana Zuberi alimwoa akiwa bado mdogo. Huenda sababu kuu iliyomfanya Amina akubali kuolewa na Bwana Zuberi ni uchumi. Amina mwenyewe anasema hataki bintiye Shemsa aolewe na kijana Dude eti kwa vile hawezi kuyatimiza mahitaji ya kiuchumi ya Shemsa Amina analalamika:

> Eee, yamekuwa makubwa! Badala ya kuolewa sisi na mwanamume, tumwowe yeye, na mali yetu iwe yake; na mshahara wa Shemsa uwe wake yeye pia, na kisha tumpe mshahara mwingine. He, si madogo; vitakuwa viroja si haba..... A-a umemchunuka vibaya Dude wako [6]

Katika riwaya ya *Utengano*, Bwana Maksuudi alimwoa Mwanasururu na baada ya kumhini mali yake, Bwana Maksuudi alimtaliki. Hapa Bwana Maksuudi alimlemaza Mwanasururu kiuchumi kitendo ambacho kinamfanya Mwanasururu kuwa wazimu na hatimaye kusababisha kifo chake. Alishikwa na ugonjwa wa akili baada ya kudhulumiwa na mumewe kwa kumnyanganya mali yake.

Wanawake wengi wamesawiriwa wakifanya uasherati si kwa sababu ya kupenda kwao bali kwa sababu ya kutojiweza kiuchumi. Tunaelezwa katika riwaya ya *Asali Chungu:*

Haja ndiyo illiyombadilisha, moyo wake mgumu ukalainika. Akakubali yale ambayo kwake yalikuwa magumu kutendeka. Akasalimu amri na kutoa lile ambalo watu walikuwa wakilichimba. [7]

Tumefafanuliwa jinsi ukosefu ulivyomfanya Semeni kukubali yale aliyokuwa akiona mwiko kwake kuyafanya. Hata Pili naye anakiri kwamba anatoka nje kwa sababu asipotoka hawezi kula. Katika *Utengano*, Kazija anachukia hali ya kumpendeza mwanamume kwa kujirembesha lakini hana hiari. Tunaelezwa;

Kwa kweli yeye hafanyi laana kupenda ila ni kwa sababu ya ukosefu [8]

Chumba ambacho amekipangiza amekinadhifisha kwa ajili ya kuwavutia wateja wake. Wateja hapa ni wanaume ambao mfumo wa kiuchumi unawapendelea na kwa hivyo kuwafanya wanawake wawe wakiwategemea.

Mama Shoka anafanya kazi ngumu ili kuweza kuwalazimu watoto wake wawili pamoja na mumewe ambaye anatumia pesa anazozipata kwenye ulevi. Mwandishi anaonyesha kupitia kwa mama Shoka kwamba ingawa wanawake wana shida za kiuchumi, kuna njia halali ambazo wanaweza kuzitumia katika kuyaendeleza maisha yao.

## 2.5 MALEZI YA MTOTO WA KIKE

Mara nyingi ukosefu wa malezi mazuri kumesababisha kuyaharibu maisha ya watoto wa kike ingawa pia wengine wamechangia katika kuyakuza. Wazazi wa kiume wamechangia suala hili kwa kufanya uamuzi kuyahusu maisha ya wanawake hata kabla ya kutafuta njia ya kumwelewa kwanza mtoto wa kike.

Kulingana na mwanafalsafa maarufu Aristotle, daima, maishani mwanamke huwa chini ya utawala wa mwanamume, utotoni mtoto wa kike huwa chini ya mzazi wa kiume na anapoolewa anakua chini ya mumewe.

Maimuna wa riwaya ya *Utengano* ni mfano mzuri wa mtoto aliyelelewa na tabia yake kukuwa kulingana na matakwa ya babake. Maksuudi anamnyima uhuru wa kutangamana na watu wengine katika jamii ili aweze kuonja uchungu na utamu wa maisha ili aweze kujichagulia njia atakayofuata.

Kwa kutoruhusiwa kutoka nyumbani Maimuna anajiona kama mfungwa. Maksuudi anafikiri kwamba anamsaidia bintiye asimezwe na ulimwengu lakini mambo hayaendi hivyo. Jinsi Maimuna alivyoukosa uhuru, alishindwa kuuelewa ulimwengu, mwishowe anapopata nafasi ya kutoroka kwao anashindwa aanzie wapi na achague gani nzuri na aache gani ambapo mtu hatambui kilichomo. Hatimaye tunamwona Maimuna anaingilia mambo ya ukahaba.

Kwa maoni yetu, kuwekwa nyumbani kwa Maimuna ni maonevu kwa mtoto wa kike. Tukimlinganisha Maimuna na nduguye wa kiume Mussa, tunaona tofauti kubwa sana katika jinsi wanavyolelewa. Mussa yuko huru kutembea na anaenda shuleni. Uhuru wa Mussa unamfanya aelewe ulimwengu hasa pale wanapofumaniana na babake nyumbani kwa Kazija. Kitendo hiki kilimfunza mengi Mussa ambaye anaamua kuyabadili maisha yake kabisa. Maimuna naye angeachwa awe huru atangamane na kujichagulia jema, labda hangeishia kuingilia mambo ya ukahaba. Kufungiwa kwake hakumsaidii katika kufanya uamuzi. Badala yake kunamsaidia katika kufanya uamuzi usiofaa.

Kuna wasichana wengi ambao wanaangamia maishani kwa sababu ya ukosefu wa sheria mwafaka. Kulelewa kwa Maimuna kunaweza kulinganishwa na kule kwa Amina wa riwaya ya *Siku Njema* ya Ken Walibora na pia Rosa Mistika wa riwaya ya *Rosa Mistika* ya Euphrase Kezelahabi.

Ingawa pia tunaona kuwa kitendo cha Biti Kocho na Farashuu kumtorosha Maimuna kinaonyeshwa kama ni cha kulipisha kisasi, aliyekosa si Maimuna bali ni babake. Kwa hivyo hapa tunaona kwamba makosa ya baba yanasababisha kuonewa kwa mtoto wa kike.

Tunalopendekeza hapa ni kwamba huku wanawake wakipigania uhuru na haki zao inafaa kwanza kabisa wapiganie kubuniwa kwa sheria zitakazowalinda watoto wasichana.

Inaonekana kwamba maisha ya baadaye ya wasichana wengi yanategemea jinsi walivyolelewa wakiwa wadogo. Kwa hivyo ikiwa kutakuwa na sheria ya kuwalinda tangu utotoni, basi watakuwa wanajielewa na vilevile kujua haki zao. Mhusika Semeni wa *Asali Chungu* haelewi haki zake na ndiyo sababu anaponajisiwa, hajui ajitetee vipi. Baada ya sheria kama hizi kubuniwa, wanawake wapiganie kuelimishwa kwa umma kuhusu sheria hizi ili ziweze kufahamika na wote yaani wake kwa waume.

Wanawake wajue hatua wanayopaswa kuchukuwa wanapodhulumiwa na pia wanaowadhulumu wajue matokeo ya dhuluma zao. Sheria tunazopendekeza wanawake wapiganie kuundwa ni pamoja na sheria kuhusu elimu ya mtoto wa kike, sheria kuhusu unajisi na kadhalika. Sheria kama hizi zitakapobuniwa, zitakuwa kama ngao ya kuwalinda wanawake. Ubaguzi kati ya watoto wa kike na wakiume kwa upande wa malezi uondolewe.

## 2.6 MWANAMKE KATIKA NDOA

Ndoa ni miongoni mwa asasi za kijamii ambazo baadhi ya wafuasi wa ufeministi wanapigania ziondolewe. Wafuasi waufeministi wanadai kwamba ndoa ni moja kati ya asasi nyingi za kijamii ambazo hutumiwa katika kuwadhulumu wanawake. Madai ya ufeministi kuhusu ndoa ni kwamba mwanamke anapoolewa na kulipiwa mahari, mwanamke huchukuliwa kuwa mali yake. Hali hii kulingana na ufeministi husababisha kuonewa na kudhulumiwa kwake. Kwa sababu ya mahari anayolipa mwanamume anaona

kuwa amemnunua mwanamke na kwa hivyo mwanamke ni mali yake. Hali kama hii imechangia pakubwa katika kuendeleza unyanyaswaji wa wanawake.

Said Ahmed Mohamed ameangalia suala hili katika *Asali Chungu* na *Utengano*. Katika *Asali Chungu*, mhusika mkuu Amina, mfano mzuri wa mwanamke katika ndoa. Ingawa Amina anasawiriwa kama mwanamke aliye huru kiuchumi, kisaikololojia anateseka. Ndoa ya Amina haimpendezi. Ameolewa na mzee ambaye si hirimu kwake.

Wanawake wengi hujikuta wameolewa na wazee wakubwa kwa sababu mbalimbali. Ni wachache sana wanaoweza kukubali kuolewa na wazee wanaowazidi umri kwa sababu ya mapenzi. Wengi hukubali kutokana na shurutisho za aina mbalimbali. Shurutisho hizo sana sana huwa ni za kiuchumi. Mwanamke anaweza kukubali kuolewa na mzee anayemzidi umri kwa sababu mzee huyo anaweza kuyagharamia mahitaji yake au hushurutishwa na wazazi wao hasa wazazi wa kiume wanaowaoza kwa sababu ya kutamani kupewa kiasi kikubwa cha mahari. Ndoa za aina hii huwa zinakosa raha.

Ndoa baina ya Zuberi na Amina ni mfano wa ndoa zilizoongozwa na suala la uchumi na hatimaye zinaishia kuwa zenye mashaka tele. Huenda ikawa Amina alishurutishwa na wazazi au tamaa yake mwenyewe kwa mali aliyokuwa nayo Bwana Zuberi Amina hatosheki wala kufurahia ndoa yake. Tunaona akilalamika;

Lakini nikijitazama miye na kitoto kile, sina kosa uso wa kumkabili. Ah!si kosa langu kwani Bwana Zuberi amenioa ningali mdogo sana na pengine umri kati yetu unanifedhehesha sana [9].

Amina haifurahii ndoa hii. Si ndoa iliyoogozwa na mapenzi, labda iliongozwa na sababu za kiuchumi. Amina anatafuta vijana barubaru ambao watatimiza haja ya kuzima ashiki zake za kimapenzi kama vile vijana Dude. Dude anamtimizia haja ambazo Bwana Zuberi hawezi kutimiza kwa sabau ya umri. Amina ni mfanao tu wa wanawake wengi wanaoolewa kwa shurutizo za aina mbalimbalina baada ya muda mfupi ndoa inakuwa yenye mashaka mengi. Baada ya muda wanawake hao wanalazimika kutafuta vijana wanaoweza kuzima kiu chao cha mapenzi na wale ambao hawawezi kujasiri kufanya kitendo kama cha Amina wanaume kisaikolojia. Hali kama hii husababisha kuvunjika kwa ndoa au mwanamke kutamani mume afe haraka ili awe huru kutafuta wapenzi watakaozima uchu wake.

Katika riwaya ya *Utengano* (1980), ndoa ya Bi. Tamima ni mfano mwingine wa madhila yanayompata mwanamke katika ndoa. Matatizo yanayomkabili Bi. Tamima ni ya aina nyingine yakilinganishwa na ya Amina wa *Asali Chungu*. Bi. Tamima hana uhuru hata wa kujiamulia kuyahusu maisha yake mwenyewe. Jambo hilo linaonekana pale Amina anapokuwa katika hali ya kutaka kujifungua, hawezi kuamua kwenda hospitalini wala kumwita mkunga yeyote kwa kuogopa adabu atakayoipata kutoka kwa mumewe Bwana Maksuudi. Isitoshe Bi. Tamima harusihiwi kutoka nyumbani. Walio na ruhusa ya kutoka nyumbani ni Bwana Maksuudi na mwanaye wa kiume Mussa. Maisha ya Bi. Tamima

katika ndoa ni sawa na ya utumwa. Haruhusiwi hata kutoka nyumbani na kutangamana na wanawake wenzake. Hata watumishi wake wana uhuru kumshinda. Mtoto wake wa kiume ana uhuru kumshinda mamake.

Bi Tamima anasema,

> Mm-mm-u...babake hataki tutoke nje ila kwa ruhusa yake na humu asiingie mtu ila kwa ruhusa yake.[10]

Madhila kama haya yanapaswa kupingwa kwa hali zozote zile. Bwana Maksuudi mwenyewe anatembea na hata kumwendea Bi Tamima kinyume. Maksuudi mwenyewe anakiri kwamba anamhini Bi Tamima kwa kuendea wanawake wengine yaani akina Kazija

> Na….Unajua Kazija ,mimi naaacha yaaangu, namhini mke waaangu kwa kukufuata wewe ,na wewe –na wewe...mpaka lini? Enn? Mpaka lini? Hutaki, hutaki?[11]

Wanawake wanaofanyiwa madhila ya aina hii ni wengi. Maksuudi amewahini wanawake wengi akiwemo Mwanasururu ambaye anachukuwa mali yake na kumwacha hohehahe huku akimzalisha mtoto. Kwa sababu ya mateso kkutoka kwa Bwana Maksuudi, Mwanasururu anakufa huku akimwacha Kabi akiwa yatima.

Yafaa wanawake wahakikishe kwamba maslahi yao katika ndoa yanashugulikiwa vilivyo katika katiba. Wanapodhulumiwa watafute uzaidizi wa kisheria badala ya kunyamanza na kuumia.

Pia wanawake wanapaswa kuelimishwa na jinsi ya kuweza kujiinua wao wenyewe kiuchumi badala ya kutegemea kwamba wataokolewa kiuchumi wakiolewa. Wapiganie kuundwa kwa jamii mpya inayotambua nafasi zao kama washirika walio katika nafasi sawa na wanaume.

## 2.7 MWANAMKE KISIASA

Mwanamke amekuwa akipuuzwa kwa muda mrefu katika mambo yanayohusiana na siasa. Siasa imekuwa ikichukuliwa kama eneo la wanaume. Hii inadhihirika pale tunapowaona wanaume wakishikilia nafasi kubwa serikalini. Hata katika ugombaji wa ubunge wanaume tu ndio wanaoshiriki ugombezi na wanawake kama wapiga kura. Hali hii inaonekana ikiwepo tangu wakati wa ukoloni na hata baada ya mkoloni kutoka. Wanawake wanabaguliwa katika karibu viwango vyote vya kisiasa.

Bwana Zuberi katika *Asali Chungu* anawakilisha wanaume wengi waliokuwa na mamlaka wakati wa ukoloni. Zuberi ni mwakilishi wa serikali ya kikoloni katika kiwango cha Wilaya. Ingawa wanawake hawakuteuliwa katika nyadhifa za uongozi, wamesawiriwa wakipinga unyanyaswaji wa aina mbalimbali. Nje ya ofisi ya DC, wanawake wamekusanyika ili kuwasilisha malalamishi yao kwa Bwana Zuberi ambaye

ndiye DC. Wanawake hawa wamechoshwa na dhuluma wanazofanya na watumishi wa Bwana Zuberi,wanawake hao hawaogopi kuja kudai haki zao.

Bi. Pili ni mfano mzuri wa wanawake walio na mwamko wa kisiasa dhidi ya utawala dhalimu. Bi. Pili amechoshwa na jinsi wanawake wanavyonyanyaswa. Analalamika;

> Macho huchoka kutazama bibi we, hasa ikiwa litazamwalo ni dharau na jeuri, na moyo hushindwa kustahimili, ikiwa linalostahimiliwa ni unyonge na uonevu. [12]

Maneno haya ya Pili yanaonyesha kuweko kwa hisia za kisiasa miongoni mwa wanawake. Wanawake hawaridhiki na jinsi hali yao ilivyo. Hawafurahii hali yao ya kinyonge. Baada ya Pili kulalamika, mwanamke mwingine anapendekeza;

> Ikiwa hatuwezi kwa vitendo, japo kwa maneno tutasema. Tutasema potelea mbali. Na mungu akipenda yana mwisho.[13]

Mwanamke huyu ana tumaini kwamba madhila wanayofanyiwa yatafika mwisho. Ni tumaini kuwa wanawake waweze kukazana bila kufa moyo hadi watakapofikia uhuru wao. Anapendekeza kwamba ikiwa kwa vitendo hawawezi kwa maneno watasema. Maneno haya ya hawa wanawake yamemchochea Pili kihisia na kumfanya amkabili DC ofisini kwa ujasiri. Pili anamwambia DC maneno yafuatayo;

walio na mwamko wa kisiasa. Kazija hapendezwi na dhuluma za wanaume dhidi ya wanawake. Maksuudi anapomwambia Kazija jinsi anavyomhini mkewe Bi. Tamina, Kazija hafurahishwi na tabia hii. Haya yanajitokeza pale Kazija anapomwambia Maksuudi;

> Na watu unawadanganya kama wewe ni Shekhe, na wengine unawadhulumu, uafriti na udhalimu kwa wanawake... na yote hayo...[16]

Kazija hafurahi kusikia kwamba Maksuudi humwacha mkewe huku akija kumtafuta yeye. Anaona hii kama dhuluma dhidi ya mwanamke. Matamshi haya yanaonyesha kwamba Kazija ana msimamo mkali wa kisiasa dhidi ya wanaume.

Hapendezwi na jinsi wanawake wanavyotendewa na wanaume. Mwandishi mwenyewe anatudokezea kuhusu tabia ya Kazija anaposema;

> Kuna mengi ambayo Kazija anayachukia. Ndiyo, anachukia... kwanza, anamchukia mwanamume. Mwanamume anamchukia kwa sababu dhahiri, nayo ni kuwa ameekwa mbele, ingawa Kazija hajui na nani. Daima atamchukia mwanamume kwa sababu hiyo.[17]

Kazija anaona kwamba nafasi aliyopewa mwanamume katika jamii haistahili na hata haoni sababu. Anaona tu hata yeye mwenyewe anambembejea mwanamume ambaye ni kiumbe kama yeye. Kazija anaichukia jamii ambayo anaonelea kwamba ndiyo imeikuza

Bwana wewe, mtukufu wa jina na tajiri mwenye uwezo... Mungu kakupa mengi, lakini kukunyima akili na maarifa.[14]

Bwana Zuberi ameshindwa kuamini kwamba maneno ya aina hii yanaweza kusemwa na mwanamke akimlenga yeye, Bwana DC. Hapa mwandishi anawachochea wanawake wasikimie huku wenzao wakidhulumiwa. Pia anataka wanawake wajue kwamba kuliko na haki waipiganie kwa vyovyote vile bila kusita au kuogopa. Pili amerudi kwa DC mara nyingi bila kukata tamaa na hata kuogopa.

Riwaya ya *Utengano* pia imebeba mifano ya wanawake walio na mwamko wa kifeministi. Wanawake wanaotambulika hapa ni Kazija na Biti Kocho. Biti Kocho amesawiriwa akimkabili Bwana Maksuudi katika harakati za kumwokoa Bi Tamima ambaye anapigwa na mumewe hata baada ya kujifungua. Kitendo cha Bwana Maksuudi ni dhuluma ya hali ya juu ambayo mwandishi anaipinga kupitia kwa Biti Kocho. Biti Kocho anamwambia Maksuudi:

> Ala, mbona mnapokaa kwenye vikuza sauti mnapiga kelele wanawake wasitawe, wanawake hivi wanawake vile. Alaaa, mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu.[15]

Biti Kocho anamwingilia Maksuudi kisiasa. Anamwambia Maksuudi kwamba wao wanaume wakiwa kwenye mikutano wanapiga domo kuhusu haki za wanawake ahadi ambazo ni za uongo. Hawazizingatii. Kazija ni mfano mwingine wa wahusika wa kike

walio na mwamko wa kisiasa. Kazija hapendezwi na dhuluma za wanaume dhidi ya wanawake. Maksuudi anapomwambia Kazija jinsi anavyomhini mkewe Bi. Tamina, Kazija hafurahishwi na tabia hii. Haya yanajitokeza pale Kazija anapomwambia Maksuudi;

> Na watu unawadanganya kama wewe ni Shekhe, na wengine unawadhulumu, uafriti na udhalimu kwa wanawake... na yote hayo...[16]

Kazija hafurahi kusikia kwamba Maksuudi humwacha mkewe huku akija kumtafuta yeye. Anaona hii kama dhuluma dhidi ya mwanamke. Matamshi haya yanaonyesha kwamba Kazija ana msimamo mkali wa kisiasa dhidi ya wanaume.

Hapendezwi na jinsi wanawake wanavyotendewa na wanaume. Mwandishi mwenyewe anatudokezea kuhusu tabia ya Kazija anaposema;

> Kuna mengi ambayo Kazija anayachukia. Ndiyo, anachukia... kwanza, anamchukia mwanamume. Mwanamume anamchukia kwa sababu dhahiri, nayo ni kuwa ameekwa mbele, ingawa Kazija hajui na nani. Daima atamchukia mwanamume kwa sababu hiyo.[17]

Kazija anaona kwamba nafasi aliyopewa mwanamume katika jamii haistahili na hata haoni sababu. Anaona tu hata yeye mwenyewe anambembejea mwanamume ambaye ni kiumbe kama yeye. Kazija anaichukia jamii ambayo anaonelea kwamba ndiyo imeikuza

tofauti kati ya wanawake na wanaume huku mwanamume akipewa hadhi ya juu akilinganishwa na mwanamke.

Kazija ni mshiriki katika ukombozi wa wanawake na pia katika kuikomboa jamii kwa jumla. Jambo hili linadhihirika wazi kule katika uwanja wa Uhuru. Ni siku ya wagombeaji uchaguzi kujielezea mbele ya wananchi. Wananchi, wanawake kwa wanaume na wadogo kwa wakubwa wamekusanyika. Kazija anayabadilisha mawazo ya watu kumhusu Bwana Maksuudi. Baada ya Bwana Maksuudi kumaliza kutoa hotuba yake, Kazija anapewa nafasi na kutoa maoni yafuatayo:

> ...Huyu Maksuudi ambaye ameshindwa kuiendesha nyumba yake ataweza kuangalia maslahi yetu? Leo mwanawe wa kiume hawajaonana mwaka. Mtoto wake mwanamke hamjui alipo, amemtoroka, amestahabu kupigwa na ulimwengu. Maaksuudi aliyemwacha mkewe kwa kisa cha kumtorosha mwanawe ati. Na huyu huyu Maksuudi aliyekuwa akimwendea mkewe kinyume. Mbali na mali aliyojilimbikizia, ingine ya unyangnyi kwa wake zake, amemnyanganya mkewe mmoja Mwanasururu mali yake na mwisho akamwacha na kusababisha kifo chake. Mengi mengi...[18]

Kazija anatoa hotuba ya kijasiri ambayo hata wanaume hawangethubutu kuitoa. Mwandishi kupitia kwa Kazija anaonyesha kwamba wanawake wakipewa nafasi wanaweza kushiriki kikamilifu katika siasa hata kuliko wanaume. Kazija anapomaliza hotuba yake, watu wanachochewa kihisia na kutamani kumwangamiza Maksuudi. Kama Kazija hangehutubia umma labda watu hawangetambua hila za Maksuudi na labda

wangempigia kura na ashinde uchaguzini. Hatimaye Maksuudi na Zanga wanashikwa na kuwekwa korokoroni kwa miaka miwili.

Kazija amesawiriwa kama mwanamke anayeielewa siasa katika jamii yake ingawa wanawake wanadharauliwa katika jamii ya mwandishi. Mwandishi amemtumia mhusika huyu ili kuwachochea wanawake wengine wasisite kuyaangazia matatizo wanayoyaona katika jamii wanamoishi. Kusawiriwa kwa Kazija jinsi alivyosawiriwa kunaonyesha kwamba Said Ahmed Mohamed anatambua umuhimu wa wanawake katika jamii wakipewa nafasi sawa na wanaume.

## 2.8 HITIMISHO

Katika sura hii tumeonyesha matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii. Katika kuyashughulikia matatizo hayo tumeyapitia kwa kuyagawa katika vipengele mbalimbali. Tuliyoyashughulikia ni pamoja na yale yanayohusiana na sheria, elimu, ndoa, uchumi, siasa na pia malezi ya mtoto wa kike.

Mbali na kuyashughulikia matatizo yanayowakumba wanawake tumeshughulikia suala la mwamko wa wanawake jinsi inavyodhihirika katika riwaya mbili za Said Ahmed Mohamed zinazohusika. Pia tumechunguza chanzo cha matatizo yanayowakabili wanawake na hatimaye tumetoa pia maoni yetu kuhusu suala hili.

## TANBIHI

1. Mohamed, S.A. (1977) *Asali Chungu* UK 5
2. (1980) *Utengano* UK 53
3. *Utengano* UK 8
4. *Utengano* UK 11
5. *Utengano* UK 7
6. *Asali Chungu* UK 61
7. *Asali Chungu* UK 45
8. *Utengano* UK 3
9. *Asali Chungu* UK 61
10. *Utengano* UK 20
11. *Utengano* UK 11
12. *Asali Chungu* UK 3
13. *Asali Chungu* UK 3
14. *Asali Chungu* UK 6
15. *Utengano* UK 12
16. *Utengano* UK 1
17. *Utengano* UK 81

# SURA YA TATU

## *KIZA KATIKA NURU NA TATA ZA ASUMINI*

## 3.0 UTANGULIZI

Kwa vile utafiti wetu unahusu nafasi ya mwanamke katika jamii jinsi anavyosawiriwa katika fasihi, tunaenda kulichunguza suala hili tukirejelea riwaya za *Kiza Katika Nuru* na *Tata za Asumini.* Ingawa tayari tumechunguza suala hili katika sura ya pili, kuna mengi ambayo huenda yakawa tofauti katika riwaya hizi.

Mwandishi anapoandika kazi fulani katika kipindi fulani huwa kuna jambo linalomwasha na tunatarajia kwamba kuna mambo mengine ambayo mwandishi ameyazungumzia katika riwaya hizi ambayo hukuyashugulikia katika riwaya tulizozishuhgulikia hapo awali.

### *3.1.1 MUHTASARI WA RIWAYA YA KIZA KATIKA NURU*

Mwandishi ameitumia familia ya Bwana Juba katika kuwasilisha maudhui na dhamira yake jinsi yanavyojitokeza katika jamii. Riwaya ya aina hii ambayo wengi wa wanahusika wake ni wa jamaa moja huitwa *Saga.*

Hadithi ya riwaya hii inaanzia kwenye ofisi ya Bwana Juba ambapo panazuka mgogoro kati ya Bwana Juba na mwanawe Mvita. Bwana Juba ni mkuu wa Mvita kazini mbali na kuwa babake. Salma ni sekretari wa Bwana Juba mle ofisini. Bwana Juba amemteua

Mvita kama mweka siri wake pale ofisini. Alipomwita mle ofisini, alitaka kumweleza juu ya mipango yake ili. Mvita asiwe akichochea umma dhidi yake. Mvita anakataa matakwa ya babake ambaye ni mkuu wake kazini. Baada ya Mvita kukataa ushawishi wa babake, Mvita anaachishwa kazi.

Kwa vile Salma alikuwa naye ameasi na kuwa miongoni mwa wafuasi wa Mvita katika harakati za kupinga unyonywaji na dhuluma katika jamii na watu kama Bwana juba, naye anaachishwa kazi kwa kizingizio cha kuwapanguza wafanya kazi. Salma anaamua kumuunga mkono Mvita katika harakati za kuhamazisha umma kuhusu haki zao. Wanafuatana na Mvita ambaye baadaye walioana wakawa bwana na bibi.

Bi. Kudura ni mkewe Bwana Juba ambaye anamdhulumu. Bwana Juba anamtesa Bi. Kudura katika ndoa. Hata wakati Mvita na Mbishi wanawe wanapomshauri aachane na dhuluma za mumewe, anasita kukubali. Mvita aliendelea kuwa mpinzani wa babake kisiasa akishikiriana na Salma mkewe hadi pale tunapomwona Bwana Juba akimtuma Shazia na kumwangamiza Mvita. Kabla ya kifo cha Mvita, Bwana Juba anamtaliki Bi. Kudura kwa kumwona kama muasi baada yake Kudura kuhamazishwa na kitendo cha Bi. Jabu ambaye alionekana haogopi wanaume.

Baada ya Bwana Juba kumuua Mvita kupitia kwa Shazia. Bi Kudura na Mbishi wanamvamia na kumuua Bwana Juba. Bi. Kudura na Salma mkewe Mvita wanatiwa korokoroni lakini Bi. Kudura anajitoa uhai mle gerezani. Salma yuko gerezani kwa

sababu ya kifo cha mumewe Mvita kitendo ambacho amesingiziwa. Mimba ya Salma inaashiria tumaini la maisha ya baadaye hata kama Mvita amekufa.

Wafuasi wa Mvita wanamtembelea Salma gerezani na kumpa moyo, kwamba ataachiliwa na wao bado ni wafuasi wake. Salma ana mimba aliyoipata kabla ya kifo cha mumewe Mvita.

### *3.1.2. MUHTASARI WA TATA ZA ASUMINI*

Mhusika mkuu Asumini katika riwaya hii ni mwanafunzi katika chuo kikuu. Amelelewa kwenye mazingira magumu ambayo yanamfanya ashindwe hata kushirikiana na wanafunzi wengine anapofika chuo kikuu. Hatimaye Asumini anashindwa kuendelea na masomo yake kwa sababu ya tata zilizomo akilini mwake. Anashindwa kuchagua kati ya maisha ya kisasa na yale ya kizamani jinsi alivyousiwa na wazazi wake. Kabla ya kuhama chuoni anamwandikia Maimuna waliyekuwa wakiishi naye barua na kumwambia kwamba ameamua kuhama chuoni na masomo yake kukomea hapo.

Anapohama kutoka chuo kikuu, Asumini haendi moja kwa moja hadi nyumbani kwao bali anakutana na Zaina ambaye wanaishi naye hadi pale Asumini anapokuwa na ugonjwa wa akili, akapelekwa hospitalini. Anamwandikia mchumba wake Sewa barua na kumwambia vile ulimwengu ulivyomdhulumu yeye miongoni mwa watu wengine wengi. Katika barua hiyo hiyo, Asumini analalamikia malezi aliyopewa na wazazi wake ambayo yalimfanya ateseke kisaikolojia maishani mwake. Pia katika barua hiyo anamshauri Sewa asiwalee watoto wake wa kike jinsi yeye Asumini akivyolelewa na wazazi wake.

## 3.2 MWANAMKE NA UTAMADUNI

Tamaduni ni mila na desturi za jamii fulani. Jamii nyingi ulimwenguni zikiwemo jamii za Afrika Mashariki zina mila na desturi fulani. Kila jamii ina mila zake ambazo huitambulisha jamii moja kutoka kwa jamii nyingine. Tamaduni za jamii nyingi zimedaiwa kuchangia katika kumnyanyasa mwanamke. Inaaminika kwamba mila na desturi nyingi, huwa zinampendelea mwanamume huku zikimdhalilisha mwanamke. Katika riwaya tunazozichunguza katika sehemu hii, tutachunguza nafasi ya tamaduni katika usawiri wa wanawake.

Katika riwaya ya *Kiza Katika Nuru*, mhusika Bi. Kudura anachorwa akiwa kama mfungwa kwenye tamaduni ambazo yeye amezishikilia, tamaduni ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangia kudhulumiwa kwake. Miongoni mwa vipengele vya utamaduni zinazomdhalilisha mwanamke ni pamoja na wasia. TUKI (1981:317) wanaeleza kuwa wasia ni maagizo ya mtu kwa mtu au watu wake ambao anataka yatimizwe iwapo atakufa au kuondoka; ni maelezo juu ya maisha anayotoa mtu kwa watu wake.

Mwanakupona alipokuwa mgonjwa, alimuusia bintiye wasia unaojulikana kama *Utenzi wa Mwanakupona*. Utenzi huu umejaa maagizo tele ya kile mwanamke anapaswa kumfanyia mumewe ili kumridhisha. Utenzi huu unaonekana kuwa na athari kubwa hadi wa leo.

Bi. Mosi mamake Kudura alipenda kuimba wimbo huu wa *Mwanakupona* ambao ni kama alikuwa akimuusia Bi. Kudura akiwa mdogo. Sehemu ya wimbo wa *Mwanakupona* ambayo Bi. Mosi alipenda kuimba na kumwachia Kudura taathira kubwa:

Keti naye kwa adabu
Usimtie ghadabu
Akinena simjibu
Itahidi kunyamaa.

Kilala sii kukuse.
Mwegeme umpapase.
Na upepo asikose.
Mtu wa kumpepea[1]

Katika wasia huu, Mwanakupona hapendekezi jinsi mwanamume naye anvyopaswa kumridhisha mwanamke. Anapendekeza wajibu wa mwanamke kwa mwanamume. Ni kama wasia huu unamdunisha mwanamke na kumfanya chombo cha kumhudumia mwanamume. Mwanamume hawajibiki kwa mkewe.

Bi. Kudura anaonekana kushikilia wasia huu kama hirizi. Yeye Kudura anadhulumiwa na mumewe lakini kwa vile hawezi kupuuza wasia wa mamake, hawezi hata kujikomboa kutoka kwenye minyororo ya ndoa iliyo na madhila mengi. Bwana Juba hamthamini mkewe Bi. Kudura baada ya kupata cheo na kuoa bibi mwingine Bi. Khaltyy. Bwana Juba sasa anamwona Bi. Kudura kama takataka.

Bi. Kudura hawezi kufanya chochote kwa sababu ya wasia aliowachiwa na mamake.

Mbishi anapochora picha ukutani na kumwambia mamake kwamba aliyemchora ni babake, Kudura anaungulika huku akimkasirikia Mbishi. Anavuta hiyo picha ili Bwana Juba asije akaikuta kule ukutani. Hapa Bi. Kudura ni kama mtumwa wa mumewe. Hataki kuona chochote cha dhihaka kuhusu mumewe ingawa hamsaidii kwa njia yoyote. Utumwa huu unasababishwa na imani kwenye tamaduni, imani ambazo zinamdhuru anayezizingatia kama vile Bi. Kudura.

Hata wakati Mvita anamtetea mamake kwa kusema kwamba yeye hana hatia, Kudura anaelekea kumkana mwanawe ili kumridhisha mumewe. Kudura anamfokea Mvita;

> Una mama we?.... kama ingalikuwa unamtaka mama, ungalimjua na kumtii baba kwanza.[2]

Kwake Bi. Kudura anaona kuwa kwa kila kitu, bwana ndiye huja kwanza na yeye huja baadaye. Anaamini kwamba mtoto hawezi kumheshimu yeye kama hajamheshimu baba. Haya yote yanatokea kwa sababu ya imani na tamaduni ambazo hazifai hata kidogo. Bi. Kudura anateseka lakini kwa imani za kitamaduni, anaona ni heri yeye kuteseka huku bwana akiridhika.

Bi. Kudura anaishi maisha magumu ingawa mumewe ni mwenye cheo na pesa nyingi. Bwana Juba hamthamini mkewe, Bi. Kudura. Kila mara, Bi. Kudura ni mtu wa kukopa

hasa anapomtarajia mumewe kumtembelea kule kijijini. Kupitia kwa Bi. Kudura, mwandishi anaonyesha jinsi imani duni za kitamaduni zinazochangia katika kumdhulumu mwanamke lakini yeye mwanamke kaona halali. Tamaduni kama hizi ndizo ufeministi unazipinga. Ufeministi unapigania kuondolewa kwa tamaduni za aina hii.

Katika riwaya ya *Tata Za Asumini*, imani za kitamaduni zimechangia pakubwa katika ukuaji wake Asumini. Imani katika jamii ya akina Asumini inatofautiana na imani zilizopo katika jamii ya akina Kudura. Huku Kudura akiusiwa na mamake kuwa, mwanamume si mtu wa kukasirishwa, tunaelezwa kwamba:

> Sewa alikuwa chembilecho cha mamake Asumini, "Shetani, Shetani mkubwa anayepaswa kuepukwa....."[3]

Babake Asumini ndiye aliye na uamuzi kuhusu uhuru wa Asumini. Ingawa mamake pia alikuwa akimwonya tangu utotoni, ni kama mamake Asumini alikuwa akitekeleza maagizo ya mumewe yaani babake Asumini. Jambo hili linadhihirika pale ambapo tunamwona mamake Asumini akimruhusu Asumini aende kupiga ndege lakini arudi mapema kama babake hajarudi. Mamake Asumini anasema:

> Nenda urudi hima kabla babako hajarudi... basi kawia tena uko, ije iwe zilizala' apa. Tena usijitie maji makuu' vyo ukanitafutia balaa...[4]

Anachoogopa hapa si kwamba mtoto wa kike hawezi kupiga ndege lakini ni Jazume ndiye mamake Asumini anamwogopa asije akaangukia mikononi mwake na labda kumnajisi. Ulinzi kama huu ukizidi, mtoto hushindwa kujichagulia lililo jema na lilo baya katika jamii yenye mambo mengi.

Kuonywa kwa Asumini mwishowe kumemfanya hata asiguswe na mwanamume ingawa alikuwa na hisia kama binadamu wengine. Asumini anateseka kisaikolojia kutokana na malezi yake mabaya. Anapoingia chuoni, hata anashindwa kushirikiana na wanafunzi wenzake. Hali hii ndiyo iliyomfanya kuacha masomo ya chuo kikuu ghafla hata bila kutarajiwa.

Wasia wa mamake kumhusu mwanamume pia unajitokeza pale ndani ya ndege wakati ilikuwa siku yake ya kwanza Asumini kuingia na kusafiri kwa ndege. Asumini alimwambia Sewa:

> Hebu,... Ondoa majikono yako ya komanzi[5]

Wasia kama huu unaweza kumfanya mtoto wa kike asisaidiwe pahali angeweza kusaidiwa. Usaidizi utamkosa msichana kwa vile kila mara atamwona mwanamume kama shetani anavyomwita mamake Asumini.

Malezi mabaya ya Asumini yanamfanya hata ashindwe kuvalia vizuri kama wasichana wengine anapoingia chuo kikuu. Baadaye Mariam ndiye anayemchagulia jinsi ya kuvaa

ili waweze kutembea pamoja. Hata Asumini aliogopa kutengeneza nywele hadi pale anapolazimishwa na Mariam. Kulingana na Asumini jinsi alivyolelewa na kuamini ni kwamba kuvalia nadhifu ni kuharibika.

Asumini anapopendekeza wafuatane na wenzake Mariam, Sewa na Daddy kwenda disco, anashindwa kucheza na wengine. Asumini amejihini mengi kwa sababu ya msingi wa malezi yake.

Zaina anayempokea Asumini baada ya kukihama chuo kukuu anamwonya Asumini kuhusu mwanamme:

> Ah, hivyo wewe inakushtua kauli yangu? Bora uviogope vitimbi vyao wanaume. Nitazame mimi hapa nilipo. Nilipojichoma katika bahari hii inayoitwa jiji, nilipokelewa kwa vitanga vya mikono na washabiki walioniahidi kunifundika kuogelea chumvini. Leo nitazame nilivyo Zaina, kidagaa kwenye bahari ya mapapa na masansuri –topasi, topasi hapa nilipo, si wa ndoa tena wala wa wapita njia. Nimebaki natapatapa na dunia bibiangu ilivyoharibika.[6]

Zaina hapa anatoa maelezo yake baada ya kushiriki na wanaume katika vitendo vya kujamiiana huku zaina akidanganywa na mwishowe kutorokwa baada ya kuchezewa kama chombo cha wanaume.

## 3.3 MWANAMKE KATIKA SIASA

TUKI (1981) katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* wanaeleza kwamba, siasa ni utaratibu wa utekelezaji au uendeshaji wa jambo kwa kutumia busara na hekima ili kufikia lengo linalotarajiwa.

Katika riwaya hizi mbili, mwandishi amewaonyesha wanawake wanaotumia busara katika kuyafanya mambo yao. Katika riwaya ya *Kiza Katika Nuru*, tunaona jinsi wanawake wanavyotumia busara katika kupigania mambo mbalimbali wanayotaka yafaulu.

Salma anatumia busara yake na kuzikataa njama za Bwana Juba pale ofisini. Bwana Juba amemshawishi Salma akubali matakwa yake lakini Salma hakukubali kwa vile ana msimamo na anajielewa yeye mwenyewe. Hata Bwana Juba anapomshauri jinsi atakavyopandisha cheo na kumwongeza mshahara hataki yeye Salma jinsi anavyomweleza Mvita:

> Babako Mvita....leo mambo yamezidi: ametaka kutumia nguvu ofisini. Amepinduka mpaka na hii si mara ya kwanza nimeshawahi kukwambia. Ametumia rai, ametumia fedha na zawadi. Ametumia ahadi za kuninyanyua kazini, ametumia vitisho na hata mwisho amewana na mimi. Nami sikumficha uhusiano wetu; lakini haikusaidia. Akang'ang'ania. Basi mimi iweje nikatembea na mzee yule? Tena bosi wangu na wako wa kazi..[7]

Bwana Juba hana haya hata baada ya Salma kumwambia kuhusu uhusiano wake na Mvita, bado anamtamani lakini Salma, kwa sababu ya werevu wake, anazikataa hila za Bwana Juba kwa vile anajua kwamba ana haki ya kuulinda mwili na heshima yake. Baada ya Mvita kuachishwa kazi na babake, pia Salma anafuata. Anapoachishwa kazi, Salma hasiti kumfuata Mvita katika harakati za kupigania ukombozi. Mvita mumewe anapohisi kukaribia kufa, Salma anakubali ombi lake Mvita kwamba chochote kikitokea, yeye Salma aziendeleze juhudi za kuukomboa umma.

Hatimaye Mvita anapokufa, Salma anafungwa korokoroni lakini hasiti kusema ukweli wa mambo kwamba aliyeua mumewe ni ba mkwe wake yaani Bwana Juba kwa kumtumia Shazia. Akiwa gerezani, wananchi wanamtembelea na kumwambia kwamba wangali pamoja naye katika juhudi za kupigania ukombozi. Mwandishi amemtumia mhusika huyu katika kuwahamasisha wanawake wasitulie bali waamke pamoja na wana jamii wengine kwa jumla ili watetee haki zao.

Mwanamke mwingine ambaye mwandishi kamtumia katika kuonyesha mwamko wa hisia miongoni mwa wanawake ni Biti Jabu. Wanapokutana na Bi. Kudura njiani wakielekea sokoni, Biti Jabu anaongea matusi kumhusu mumewe ambaye kaoa bibi mwingine. Bi. Jabu hasiti kumchongoa mumewe. Yeye yu huru. Ameachiliwa na tamaduni ambazo humdhalilisha mwanamke.

Biti Jabu hataki kustahimili matusi kutoka kwa mwanamume muuza nyama. Muuza nyama anapomtusi Biti Jabu na kumyima nyama, Biti Jabu analichukuwa shoka na

kutaka kumkata. Biti Jabu anafanya hivi kwa sababu anaona kwamba muuza nyama anamdharau eti kwa sababu yeye ni mwanamke. Biti Jabu anamwambia:

> Mpimie bwana'ako, kama huitaki roho yako... wallahi sirudi nyuma, labda niwe mwanaharamu wa kibwana. Kama sitakuchanja mzima mzima usiniite kwa jina langu. Kwa nini mtuchezee namna hii? Kwa kuwa tunanyamaza kimya? Tukinyamaza kimya mnaona hayatuumi siyo?[8]

Biti Jabu hapa ametumiwa na mwandishi kuwasilisha malalamishi ya wanawake wengi ambao wanadhulimiwa kwa njia moja au nyingine lakini hukimya.

Kisa hiki cha Biti Jabu kilimchochea Bi. Kudura ambaye kwa miaka mingi tangu kuolewa hajawahi kumkaidi mumewe. Anaporudi nyumbani, Bi. Kudura hayavumilii tena manyanyaso ya Bwana Juba. Bi. Kudura karibu ampige mumewe ambaye kwa muda mrefu amekuwa akimheshimu kwa sababu alizingatia wasia wa mamake ambaye pia aliurithi kutoka kwa wengine waliomrithi kutoka kwa Mwanakupona.

Bwana Juba anamwambia Bi. Kudura aione nyumba yake paa. Bi. Kudura anatalikiwa na baada ya kupata talaka, anawafuata watoto wake Mvita na Mbishi. Wanaishi pamoja na pia anakuwa mshiriki mkubwa katika kuutafuta ukombozi wa nchi nzima. Bi. Kudura sasa anajasiri na kumkubali Mvita mwanawe ambaye hapo awali alimkataa eti kwa sababu alikuwa mpinzani wa mumewe yaani Bwana Juba. Hatimaye Kudura anamwambia mwanawe mvita;

Siwezi kuyafahamu kwa ukamilifu anavyosema Mvita, lakini nia yako mwanangu nimeshaiona. Nia yako kwa watu kama sisi...nitakuwa Nawe heri au shari[9]

Kubadilika kwa watu kama Bi. Kudura ni ushindi kwa wanawake. Ni kuonyesha kwamba hatimaye wanawake watatambua adui wao na kumkabili ipasavyo. Ikiwa Kudura alibadilika jinsi ile, basi kila mwanamke ako katika nafasi ya kuweza kukombolewa kisaikolojia na kuamka kuutafuta uhuru.

Katika *Tata za Asumini,* tunamwona Asumini akichukuwa pesa za wanaume na kuwachezea akili. Ingawa alikuwa akipata pesa nyingi, hakuwahi kulala na mwanamume yeyote. Aliwachukia. Pia tunamwona Asumini akimpiga Daddy chupa na kumfanya atokwe damu. Huu ni ujasiri dhidi ya mwanamume kulingana na kumbukizi za Asumini, hakuna tofauti kati ya mwanamume na mwanamke isipokuwa tofauti za kimaumbile. Asumini anayakumbuka maneno yaliyosemwa na mhadhiri wake wake pale alipokuwa katika chuo kikuu:

> Mwanamke ana tofauti kadhaa za kimaumbile na mwanamme, lakini yaliyobaki ni sawa, lakini yaliobaki ni sawa na mwanamume. Jamii zetu zinapoteza vipawa na nguvu kubwa kwa kumweka nyuma mwanamke na kumnyima haki zake na kumfanya chombo cha kustarehe au cha kuendesha maisha au kujenga

utajiri…mwanamke anaweza kufanya lolote lisilo dhidi na maumbile yake ambalo mwanamme anaweza kufanya na pengine mwanamke anaweza zaidi…[10]

Hapa Said Ahmed Mohamed amemtumia mhadhiri katika kuwasilisha ujumbe kwamba mambo mengi yanayofanywa na wanaume yanaweza kufanywa na wanawake na hata wanawake wayafanye vizuri zaidi. Hapa mwandishi anapendekeza kutambuliwa kwa usawa kati ya wanawake na wanaume katika nyanja mbalimbali. Tofauti anayoiona mwandishi ni moja tu yaani tofauti ya kimaumbile.

Asumini akiwa katika mkutano wa akina mama ambapo yeye akiwa ni miongoni mwa viongozi anashangaa kwa nini Mariam ambaye ni msomi aolewe na Mzee Mkejel jambo ambalo Asumini analiona kuwa linasababishwa na na pesa alizonazo mzee huyu.

Anashangaa kwamba semina na mijadala ilikuwa ya kitoto kwa vile wanayoyajadili hawayazingatii. Kulingana na Asumini, mwanamke hapaswi kumpenda mwanamume kwa sababu ya pesa. Asumini anasema'

> Nimesema nini kwani? Nimesisitiza tu kwamba tabia za wanaume na wanawake kwa kiwango kikubwa huimarishwa na jamii – yaani tokea wazee nyumbani, kijijini, shuleni, chuoni na katika mazingira ya maisha halisi. Nikasema, kudai haki za wanawake au hata za wanaume bila kuzingatia taathira hizo ni kazi bure[11]

Kulingana na maelezo ya Asumini kwenye mkutano, tabia ambayo watu wanakuwa nayo inatokana na jamii. Jamii haiwezi kupuuzwa katika harakati za kupigania haki kwanza kulingana na Asumini jamii ibadilishwe kwa kubadilisha asasi mbalimbali zinazokuza na kuimarisha tabia.

## 3.4 MWANAMKE KIELIMU

Kama ilivyosisitizwa na waasisi wa ufeministi, elimu ni kitu cha msingi kabisa katika harakati za kupigania ukombozi wa mwanamke. Wollstonecraft alisisitiza umuhimu wa kuwapa watoto wa kike elimu sawa na watoto wa kiume. Katika jamii nyingi vile tulivyotaja hapo awali, elimu kwa watoto wa kike si ya lazima. Hii ni kwa sababu wahusika wengi tunaowaona katika riwaya hizi hawajasoma. Kutosoma kwa wahusika wengi wa kike katika riwaya hizi hakumaanishi kwamba wanawake si werevu. Hali hii inaonyesha jinsi wanawake walivyodhulumiwa kwa kunyimwa nafasi za elimu. Hata hivyo, kuna mifano inayodhihirisha kwamba mwanamke akipewa nafasi sawa ya elimu pamoja na mwanamme, anaweza kustawi vizuri na hata kumshinda mwanamume.

Katika riwaya ya *Kiza katika Nuru* (1988), Mwajuma ni mfano wa wasichana waliosoma hadi kufikia kiwango cha chuo kikuu. Mwajuma hapa anaonyesha ukweli ya kwamba wanawake wanaweza kufanya chochote kile ambacho wanaume wanaweza kufanya.

Katika *Tata za Asumini* (1990), Mariam na Asumini ni wasichana walio katika chuo kikuu ingawa baadaye Asumini haakuendelea na masomo yake huko chuoni. Hata hivyo, wahusika wa kike waliosawiriwa kama wasomi katika riwaya hizi ni wachache mno.

## 3.5 MWANAMKE KIUCHUMI

Bado mwanamke hajapewa nafasi inayofaa katika nyenzo za uzalishaji wa mali. Mfumo wa kiuchumi bado unampendelea mwanamme. Hali hii inadhihirika kwa njia mbalimbali.

Kwanza Bi. Kudura wa *Kiza katika Nuru* ni mwanamke ambaye amedhulumiwa kiuchumi. Huku mumewe akiloa kwenye pesa na bibi wa pili Bibi Khalityy, Kudura alowa kwenye dimbwi la umasikini. Tunamwona akikopa kila mara hali ambayo inawafanya wanawake wengine wamdharau. Biashara wanazozifanya wanawake hawa. Pia biashara hizi ni duni kwa vile haziwaletei faida ya kutosha.

Kutojiweza kiuchumi kunawafanya wanawake wengi kufanya kazi ya ukahaba. Miongoni mwao ni Rose katika *Kiza Katika Nuru* anayesema:

> Bibi we, tusipowaparamia wanaume maungoni nani atatubeba katika ulimwengu huu mgumu?[12]

Rose anasema hapa kwamba, kama hawezi kuwa karibu na wanaume hawezi kula kwa vile wanaume ndio walio na pesa. Hali hii inawafanya wanawake wazidi kuwategemea wanaume jambo ambalo linasababisha kuchelewa kwa ukombozi wa wanawake.

Katika riwaya ya *Tata za Asumini* kuna wahusika waliosawiriwa kama makahaba miongoni mwao wakiwa Zaina, Masika na Mwatima. Ingawa Asumini haonani na wanaume kimwili, naye pia anapokea pesa kutoka kwao na tena nyingi zaidi.

Mariam pia hata kama amesoma, bado hajajikomboa kiuchumi ndio maana anakubali kuolewa na Bwana Mkejel ambaye ni tajiri na mzee kwa umri. Kulingana na Woolf, mwanamke atakombolewa baada ya kuwa huru kiuchumi. Aina zingine za uhuru zinautegemea uhuru wa kiuchumi.

## 3.6 HITIMISHO

Katika sura hii, tumeyaangazia masuala yanayowahusu wanawake katika riwaya za *Kiza katika Nuru* na *Tata za Asumini*.

Tuliyoyaangazia katika riwaya hizo ni pamoja na muhtasari wa riwaya hizo zote mbili, suala la mwanamke na utamaduni, mwanamke katika siasa, mwanamke kielimu na hatimaye mwanamke kiuchumi.

Ingawa tulikuwa tumeyashughulikia masuala haya katika sura ya pili, tumejaribu kadiri ya uwezo wetu kujiepusha na kuyarudia maudhui yaliyojitokeza katika sura ya pili.

# TANBIHI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mohamed, S.A, (1988) | *Kiza Katika Nuru* | UK 47-48. |
| 2. | | *Kiza Katika Nuru* | UK 44. |
| 3. | Mohamed, S.A. (1990) | *Tata La Asumini* | UK 14. |
| 4. | | *Tata La Asumini* | UK 27 |
| 5. | | *Tata La Asumini* | UK 30 |
| 6. | | *Tata La Asumini* | UK 66 |
| 7. | | *Kiza Katika Nuru* | UK 4 |
| 8. | | *Kiza Katika Nuru* | UK 110 |
| 9. | | *Kiza Katika Nuru* | UK 246 |
| 10. | | *Tata La Asumini* | UK 76 |
| 11. | | *Tata za Asumini* | UK 119 |
| *12.* | | *Kiza Katika Nuru* | UK 233 |

# SURA YA NNE

## *KUSAWIRIWA KWA WANAWAKE*

## 4.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tunachunguza jinsi Said Ahamed Mohamed amewasawiri wahusika wa kike katika riwaya zake. Kusawiri ni kuonyesha tabia ya mhusika kupitia kwa matendo yake na pia kutokana na jinsi anavyoingiliana na wanajamii wenzake. Mhusika wa kifasihi hupewa sifa mbalimbali ambazo husaidia kuwasilisha mawazo Fulani. Mwandishi hutumia mbinu mbalimbali katika kuelezea tabia za wahusika wake. Said Ahmed Mohamed ametumia njia mbalimbali katika kuonyesha taswira ya mhusika wa kike katika riwaya zake

Kwanza amewatumia wahusika wenyewe. Hapa amewatumia wahusika katika kujifafanua wenyewe jinsi wanavyojihisi. Kwa kuzingatia mbinu hii , tutaona jinsi mhusika wa kike anavyosaidia katika kuonyesha hali yake mwenyewe pamoja na hali za wanawake wenzake.

Njia ya pili ambayo itasadia katika kutambua jinsi wanawake walivyosawiriwa ni kupitia kwa wahusika wa kiume . Hapa mwandishi anamtumia mhusika wa kiume katika kumfafanua mhusika wa kike. Aidha, mwandishi amezionyesha tabia za wahusika wa kike kutokana na jinsi wanavyoingiliana na wahusika wa kiume. Kupitia kwa mhusika wa kiume mwandishi huonyesha jinsi wanaume wanavyowachukulia wanawake.

Njia nyingine ambayo mwandishi anaitumia katika kubainisha na kufafanua tabia ya mwanamke ni kupitia kwa maelezo yake mwenyewe. Hapa mwandishi mwenyewe anachukuwa fursa ya kumfafanua mhusika katika kusistiza wazo fulani ambalo angependa kuwasilisha kupitia kwa mhusika huyo .

Katika riwaya zake, Said Ahmed Mohamed amemsawiri mwanamke katika jamii kwa njia mbalimbali. Kwa vile uhakiki wetu unajikita kwenye maudhui ya kifeministi, tutachunguza mchango wa aina mbalimbali za usawiri wa mwanamke katika kufanikisha malengo ya uhakiki wa kifeministi. Katika riwaya za Said Ahmed Mohamed picha ya mwanamke katika jamii imejitokeza katika sura mbalimbali ambazo tunazishughulikia moja baada ya nyingine. Tutazigawa katika makundi mbalimbali ili ziweze kubainika wazi.

## 4.1 MWANAMKE KAMA MDHULUMIWA

Mwanamke katika riwaya za Said Ahmed Mohamed amejitokeza kama mtumwa wa mwanamume. Hali hii ya dhuluma za mwanamume kwa mwanamke inajitokeza katika riwaya zote za Said Ahmed Mohamed ambazo tumezishughulikia katika tasnifu hii, yaani *Asali Chungu* (1977), *Utengano* (1980), *Kiza Katika Nuru* (1988) na *Tata za Asumini* (1990). Katika kumsawiri mwanamke kama mdhulumiwa, mwandishi ameonyesha asasi mbalimbali ambazo huchangia katika kudhumiwa kwa mwanamke. Baadhi ya asasi tunazoenda kuzungumzia jinsi zinavyojitokeza katika riwaya hizi ni kama vile,mwanamke kama mfanya kazi, mwanamke katika ndoa na malezi ya mtoto wa kike.

### 4.1.1 KUDHULUMIWA KAMA MFANYA KAZI

Katika riwaya za Said Ahmed Mohamed, mwanamke mfanya kazi amesawiriwa kama mdhulumiwa. Mwananamke anafanya kazi katika mazingira yasiyofaa na yenye wasiwasi mwingi. Mifano mizuri ya wanawake wanaodhulumiwa kama wafanya kazi ni pamoja na Salma wa *Kiza katika Nuru* na Semeni wa *Asali Chungu*. Wahusika hawa wametumiwa na mwandishi katika kuyawasilisha matatizo yanayowakumba wanawake wanapokuwa wakifanya kazi chini ya wanaume. Katika hali kama hii, mwanamume hutumia uwezo na mamlaka yake katika kumdhulumu mfanya kazi wa kike.

Salma wa *Kiza katika* Nuru ni mwanamke anayefanya kazi chini ya Bwana Juba. Salma ni mchumba wa Mvita ambaye ni mtoto wa Bwana Juba. Kwa vile Salma anafanya kazi chini ya Bwana Juba, Mzee huyu anaonekana akimshawishi Salma akubali kutumiwa kama chombo cha kuuzima uchu wake. Salma hawezi kunyanyuliwa kimadaraka mle ofisini kabla ya kuitikia matakwa ya Bwana Juba, ingawa Salma tayari amemwelezea kuhusu uhusiano wake na Mvita mwanaye,Bwana Juba hataki kukubali kwa vile anajiona mkubwa na lolote alitakalo anapaswa kulipata bila pingamizi yoyote. Salma anamweleza Mvita vile Bwana Juba alivyotaka kumnajisi mle ofisini. Anamwambia:

> Babako Mvita Leo mambo yamezidi; ametaka kutumia nguvu ofisini. Amepindukia na hii si mara ya kwanza nimeshawai kukwambia. Ametumia rai, ametumia fedha na zawadi. Ametumia ahadi za kuninyanyua kazini, ametumia vitisho na hata mwisho amewana na mimi. Nami sikumficha uhusiano wetu; lakini haikusaidia. Akang'ang'ania.Basi mimi iweje nikatembee na mzee yule? Tena bosi wangu na wako wa kazi...[1]

Katika mazingira kama haya , mwanamke anadhulumiwa kwa vile hawezi kupandishwa madaraka kama hajatimiza matakwa ya mwanamume ambaye ni bosi wake kazini . Hali kama hii hupelekea kuachishwa kazi kwa mwanamke asiyetii amri ya bosi wa kiume.

Mazingira anayofanya kazi Salma pia yanaonyesha kwamba mabosi wa kiume hawawachii wafanya kazi wa kike uhuru wa kujiamulia yale yaliyo mema kwao kuyazingatia. Kwa vile Salma anakataa kuitikia maombi ya Bwana Juba na pia kuamua kuwa mfuasi wa Mvita anayempinga babake, anaachishwa kazi.

Dhuluma kama hizi za Bwana Juba kwa Salma zinapaswa kupingwa kwa vyovyote vile. Sheria zibuniwe ambazo zitawalinda wanawake kazini kutokana kwa hila za wakuu wao wa kiume.

Mfano mwingine wa mwanamke anayedhulumiwa kama mfanya kazi ni ule wa Semeni wa riwaya ya *Asali Chungu*. Semeni ni mfanya kazi wa nyumbani kwa Bwana Zuberi .

Bwana Zuberi anatamani sana kuuzima uchu wake wa kimwili kwa Semeni lakini Semeni ni mgumu, hataki kuitikia ombi la Bwana Zuberi. Semeni anaithamini sana heshima yake kuliko pesa anazoahidiwa na Bwana Zuberi kupitia kwa Biti Daudi. Mwandishi anatoa maelezo yafuatayo kuhusu msimamo wa Semeni;

> Kwa Semeni, ilikuwa bora kung'ang'anua masufuria akapata angalau tonge, kuliko kupewa tunu za aina kwa aina kwa, alichokiona mwenyewe; uchafu [2]

Kitendo cha Bwana Zuberi cha kumnyemelea na kumnajisi Semeni ni dhihirisho la dhuluma za hali ya juu kwa mwanamke kama mfanya kazi. Bwana Zuberi anatenda kitendo cha kinyama kwa kumvunjia heshima Semeni ambayo kwa muda mrefu ameithamini.

Kupitia kwa wahusika Salma na Semeni, Said Ahmed Mohamed ameyaangazia na kuyaweka wazi matatizo ambayo mwanamke huyapitia kama mfanya kazi. Kama tulivyodokezea hapo juu dawa ya pekee ya kutibu ugonjwa wa aina hii unaowakumba akina Zuberi na Juba ni kubuniwa kwa sheria zitakazomtetea mwanamke kama mfanya kazi. Sheria za aina hii zipendekeze kuchukuliwa kwa hatua kali dhidi ya bosi yeyote atakayemdhulumu mfanya kazi wa kike kwa njia yoyote ile.

### 4.1.2 DHULUMA KATIKA NDOA

Taasisi nyingine ambayo Said Ahmed Mohamed ameitumia kuyaangazia madhila ya wanaume dhidi ya wanawake ni ndoa. Mwandishi ametumia ndoa mbalimbali katika kuwasilisha picha ya maisha ya mwanamke katika ndoa. Ndoa nyingi ambazo mwanandishi anazitumia katika riwaya zake zina matatizo na anayedhurika zaidi katika ndoa yenye mizozo ni mwanamke.

Katika ndoa nyingi ambazo mwandishi amezitumia, mwanamke amesawiriwa kama mtumwa wa kumhudumia mwanamume. Mwanamke hata hayuko huru kujiamulia kuhusu jambo lolote maishani.

Bi. Tamima wa *Utengano* ni mfano mzuri wa mwanamke anayedhulumiwa katika ndoa. Bi. Tamima amewekwa katika kiwango sawa na bintiye kwa kutoruhisiwa kutoka nyumbani. Hali hii tunatambua kupitia kwa malalamishi ya Bi. Tamima kwa Maimuna;

> Mm-u, Mm-u... babako hataki tutoke nje ila kwa ruhusa yake, na humu asiingie mtu ila kwa ruhusa yake [3]

Mbali na kutoruhusiwa kutoka nje, Bi. Tamima haruhusiwi hata kujiamulia mwenyewe kuyahusu maisha yake hasa pale anapokuwa karibu kujifungua. Kupigwa anakopigwa Bi.Tamima, ni kama msisitizo wa baadhi ya madhila makubwa wanayoyapitia wanawake wakiwa katika taasisi ya ndoa.

Mwanasururu ni mfano mwingine wa mwanamke ambaye Bwana Maksuudi anamdhulumu katika ndoa kitendo ambacho kinasababisha maradhi ya akili yanayomkumba Mwanasururu na hatimaye anakufa. Tunaambiwa kwamba hata kabla Bwana Maksuudi amwoe Mwanasururu, Mwanamke huyu alikuwa na mali yake. Baadaye Bwana Maksuudi alimhini mali yake Mwanasururu vile anavyosema Kazija:

> ... mbali na mali alipojilimbikizia, nyengine ya unyanganyi kwa wake zake. Amemnyanganya mkewe mmoja, Mwanasururu mali yake na mwisho akamwacha na kusababisha kifo chake.[4]

Mwanamke mwingine anayesawiriwa akidhulumiwa katika ndoa ni Bi. Kudura wa *Kiza Katika* Nuru. Wasia alioachiwa na mamake Bi. Mosi alimpendekezea kile alichopaswa kumtekelezea mumewe kupitia kwa wimbo wa Mwanakupona. Bi. Kudura akakuwa kiumbe wa kumnyenyekea mwanamume tabia ambayo anaishikilia hadi pale anapokutana na Bi. Jabu anayemzindua na kumfanya aone jinsi amekuwa akidhulumiwa kwa muda mrefu.

Dhuluma nyingine dhidi ya mwanamke ni ile ya mwanamke kuolewa na mzee aliyemzidi maradufu kwa umri. Ndoa ya aina hii humfanya mwanamke kuteseka kisaikolujia kwa vile anahitaji mume waweze kufurahia ndoa yao. Mfano wa utumwa wa aina hii ni wa ndoa baina ya Bwana Zuberi na Bi. Amina. Kwa vile Amina hatosheki na mumewe ambaye ana umri mkubwa kumliko, anawatafuta vijana barubaru walio na nguvu za

kuweza kumtimizia haja zake za kimwili. Ndoa hii imesawirwa kuwa labda ilisababishwa na mali aliyonayo Zuberi.

### 4.1.3 *KUDHULUMIWA KWA MTOTO WA KIKE*

Mwandishi pia ameyasawiri malezi ya mtoto wa kike kama jambo lililo muhimu sana maishani na ikiwa mtoto atalelewa vibaya au adhulumiwe katika malezi, maisha ya mtoto huyo huenda yakawa yenye mashaka mengi. Mifano ambayo mwandishi ametoa kuonyesha madhara yanayoweza kumfika mtoto wa kike kama hajalelewa vizuri ni pamoja na Maimuna wa *Utengano* na Asumini wa *Tata za Asumini.* Maimuna na Asumini wanadhulumiwa katika malezi.

Mwandishi anaelekea kumlaumu babake Maimuna kwa kitendo cha kuingilia ukahaba. Kupitia kwa Maimuna na babake, mwandishi anaonyesha tabia ya wazazi wengi wa kiume ya kutowaelewa watoto wao wa kike na hivyo kuwafanyia uchaguzi usiofaa ambao mwishowe unayaharibu maisha yao.

Asumini akiwa mdogo, anaonywa dhidi ya kumkaribia mtoto wa kiume. Kulingana na wazazi wake Asumini, mtoto wa kiume ni shetani ambayo msichana hafai kuwa karibu naye. Katika riwaya ya Tata *Za Asumini*, Asumini anapokuwa mkubwa anashindwa jinsi ya kushirikiana na vijana wengine. Kitendo hiki cha kumfanya awaogope wavulana kinasababishwa na kule kunyimwa nafasi ya kuwaelewa na hivyo Asumini kushindwa kukubali hata Sewa ambaye anataka kumuoa. Hatimaye Mawazo mengi yanamfanya Asumini augue ugonjwa wa akili na kupotea.

## 4.2 MWANAMKE KAMA KAHABA

Said Ahmed Mohammed amewasawiri wahusika wengi wanawake kama makahaba. Anapowasawiri wahusika hawa, anatoa sababu zilizowafanya wahusika hao waingilie kazi ya ukahaba. Kupitia kwa wahusika wakuu ambao mwandishi amewasawiri kuingilia ukahaba kutokana na shurutisho mbalimbali, tunaweza kuchukulia kwamba shurutisho za aina hii ndizo huwafanya wanawake wengi kushiriki katika biashara ya ukahaba.

Wahusika wakuu ambao mwandishi amewasawiri wakiingilia mambo ya ukahaba kwa sababu mbali mbali ni pamoja na Amina, Semeni, Bi. Pili (Asali Chungu), Maimuna (Utengano), Zaina (Tata Za Asumini) na Rose (Kiza Katika Nuru).

Mwandishi anamsawiri Amina katika *Asali Chungu* akiingia kwenye ukahaba kwa vile yeye bado ni mbichi na mumewe amekuwa mzee ambaye hawezi kumtimizia haja zake za kimapenzi. Kupitia kwa Amina, mwandishi anatudokezea athari zinazosababishwa na ndoa baina ya watu walio na tofauti kubwa ya umri kati yao, labda ndio iliyoshawishiwa na pesa au shurutisho za aina nyingine.

Semeni wa *Asali Chungu* pia ni kahaba. Mhusika huyu amelamizika kuingilia mambo ya uasherati kwa sababu ya kitendo cha Bwana Zuberi kumnajisi na kumtunga mimba ambayo baadaye inasababisha kuzaliwa kwa Dude. Kwa vile kiuchumi Semeni hajiwezi, anashurutishwa kuingilia mambo ya ukahaba ili aweze kujikimu na pia kumkimu mwanaye Dude.

Bi. Pili katika *Asali Chungu* naye ni mshiriki kwenye biashara ya ukahaba. Anashiriki ukahaba ili yeye na mtoto wake waweze kupata mtaji.

Maimuna *(Utengano)* anatoroka maisha ya kitumwa katika nyumba yao. Kwa vile hajawahi kutoka nyumbani na kutambua jinsi maisha yalivyo, anapotoroka, Maimuna anatumbukia kwenye shimo la ukahaba. Sababu iliyomfanya Maimuna kuishia kwenye ukahaba si ya kiuchumi bali uhuru alionyimwa na babake Bwana Maksudi.

Katika Tata Za Asumini mwandishi amemsawiri Zaina kama kahaba. Naye anashiriki ukahaba pamoja na wenzake ili aweze kupata namna ya kujikimu.

Pia katika riwaya ya *Kiza Katika Nuru*, Rose amesawiriwa akijitafutia mtaji kutokana na vitendo vya kisherati.

## 4.3 MWANAMKE KAMA MWANASIASA

Baada ya kuwasawiri wahusika wa kike kama wadhulumiwa, mwandishi pia anawasawiri wahusika wengine katika juhudi za kuwakomboa wanawake wenzao wanaodhulumiwa. Hawa wanawake wanaowakomboa wenzao ni wale ambao wamepata mwamko, kutambua haki zao na kuamua kuzipigania haki zao na za wanawake wenzao. Sababu ya mwandishi kuwasawiri wahusika wa aina hii ni kuwahamazisha wanawake ili wasikimbie wakati wanapodhulumiwa bali wapiganie haki zao.

Bi. Pili katika *Asali Chungu* naye ni mshiriki kwenye biashara ya ukahaba. Anashiriki ukahaba ili yeye na mtoto wake waweze kupata mtaji.

Maimuna *(Utengano)* anatoroka maisha ya kitumwa katika nyumba yao. Kwa vile hajawahi kutoka nyumbani na kutambua jinsi maisha yalivyo, anapotoroka, Maimuna anatumbukia kwenye shimo la ukahaba. Sababu iliyomfanya Maimuna kuishia kwenye ukahaba si ya kiuchumi bali uhuru alionyimwa na babake Bwana Maksudi.
Katika Tata Za Asumini mwandishi amemsawiri Zaina kama kahaba. Naye anashiriki ukahaba pamoja na wenzake ili aweze kupata namna ya kujikimu.

Pia katika riwaya ya *Kiza Katika Nuru*, Rose amesawiriwa akijitafutia mtaji kutokana na vitendo vya kisherati.

## 4.3 MWANAMKE KAMA MWANASIASA

Baada ya kuwasawiri wahusika wa kike kama wadhulumiwa, mwandishi pia anawasawiri wahusika wengine katika juhudi za kuwakomboa wanawake wenzao wanaodhulumiwa. Hawa wanawake wanaowakomboa wenzao ni wale ambao wamepata mwamko, kutambua haki zao na kuamua kuzipigania haki zao na za wanawake wenzao. Sababu ya mwandishi kuwasawiri wahusika wa aina hii ni kuwahamazisha wanawake ili wasikimbie wakati wanapodhulumiwa bali wapiganie haki zao.

Wanawake ambao mwandishi amewatumia katika kutetea haki za wenzao wanaodhulumiwa ni pamoja na Binti Kocho na Kazija wa *Utengano*, Bi Pili wa *Asali Chungu*, Binti Jabu wa *Kiza Katika Nuru*, na Mariam wa *Tata Za Asumini*.

Biti Kocho amesawiriwa na mwandishi akiyaangazia matatizo yanayomkumba Bi. Tamima na Bintiye Maimuna chini ya ulinzi dhalimu wa Mzee Maksuudi. Biti Kocho anamkabili Bwana Maksuudi bila uoga na kumwambia kwamba jinsi anavyowatendea Bi. Tamima na binti yao Maimuna si halali. Ingawa Biti Kocho pia anawakilisha kundi la wanawake ambao wanaelewa haki zao katika kazi. Mwandishi anawashauri wanawake kupitia kwa Biti Kocho kwamba wana haki ya kutoa maoni yao katika hali yoyote ile.

Bi. Pili wa *Asali Chungu* naye amesawiriwa kama mtetezi wa haki za wanawake. Anamlalamikia Bwana Zuberi, DC kuhusu dhuluma yake kwa Semeni. Bi. Pili ni mwanamke anayeilewa jamii na dhuluma ambazo viongozi wanawafanyia wanawake.

Binti Jabu wa *Kiza Katika Nuru* naye ni mwanamke ambaye mwandishi amemtumia kuwachochea wanawake wengine. Kupitia kwa Binti Jabu, Bi. Kudura anazinduka kutoka gizani. Anamtambua kwamba amekuwa akiishi kama mfungwa na hivyo anahitaji uhuru. Bi. Kudura anazinduliwa na kile kitendo cha Biti Jabu kumtolea maelezo kuhusu mumewe ambaye pia ana bibi mwingine kama Bwana Juba.mumewe Kudura.

Kitendo cha Biti Jabu kumkabili muuza nyama kinamchochea zaidi Bi. Kudura ambaye anatambua kwamba kumbe wanawake pia wanaweza kukabilinana na wanaume. Kudura

anaporudi kwake, anamkabili mumewe kwa njia tofauti kabisa ambapo anataka hata kumpiga. Hali hii imechochewa na Biti Jabu. Hatimaye Bwana Jabu anamtaliki Bi. Kudura ambaye anaungana na watoto wake Mvita na Mbishi katika kupigania ukombozi wa jamii. Hatimaye anamuua Bwana Juba huku wakishirikiana na Mbishi. Kubadilika kwa mawazo ya Bi. Kudura ni dhihirisho kwamba, mwanawake anayedhulumiwa akipata kuzinduka anaweza kuwa mkali zaidi.

Mariam wa *Tata Za Asumini* pia ni mfano mwingine wa mwanamke aliyekombolewa kimawazo. Yeye anashiriki dansi lakini si kwa kuharibika bali kwa kustarehe kama watu wengine, yeye ndiye anamfunza Asumini jinsi ya kuvalia vizuri.

## 4.4 HITIMISHO

Katika sura hii, tumechunguza jinsi Said Ahmed Mohamed alivyowasawiri wanawake katika riwaya zake. Baada ya kueleza jinsi wanawake walivyosawiriwa, tumeeleza sababu za kumfanya mwandishi kuwasawiri jinsi alivyowasawiri.

Tuliyoyazingatia katika maelezo yetu juu ya usawiri wa wanawake ni pamoja na mwanamke kama mdhulumiwa, mwanamke kama kahaba na pia mwanamke kama mwanasiasa.

Katika kuangazia usawiri wa mwanamke kama mdhulumiwa tumeangazia dhuluma za mwanamke katika ndoa, dhuluma katika kazi na pia dhuluma katika malezi ya watoto wa kike. Katika kuangazia dhuluma katika ndoa, jinsi mwandishi amemsawiri mwanamke,

tumewatazama wahusika kama vile Amina wa *Asali Chungu,* Kudura wa *Kiza Katika Nuru* na Bi. Tamima na Mwanasururu wa *Utengano.* Upande wa mwanamke akidhulumiwa kama mfanyakazi, tumewatazama, Semeni wa *Asali Chungu* na Salma wa *Kiza Katika Nuru.*

Usawiri wa mwanamke kama mdhulumiwa katika Malezi, tumemtazama Maimuna wa *Utengano* na Asumini na *Tata Za Asumini.*

Tena tumemwangalia mwanamke jinsi alivyosawiriwa kama kahaba na kutoa sababu tulizofikiri zilimfanya mwandishi kumsawiri mwanamke kwa jinsi hiyo. Wahusika tuliowaangalia ni pamoja na Semeni, Maimuna, Zaina na Rose.

Mwisho tumemwangalia mwanamke kama mwanasiasa ambapo tumewatazama
Bi. Pili wa *Asali Chungu*, Kazija na Biti Kocho wa *Utengano*, Biti Jabu wa *Kiza Katika Nuru* na Mariam wa *Tata Za Asumini.*

## TANBIHI

1. Mohamed, S.A (1988) *Kiza katika Nuru* UK. 4
2. ___________ (1977) *Asali Chungu* UK18
3. ___________ (1980) *Utengano* UK 20
4. ___________ *Utengano* UK 81

# SURA YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

Kwa kuhitimisha kazi hii, tunaenda kuangalia kwa ufupi yale tuliyoyajadilia katika sura za kwanza nne. Tena tutaangalia kufaulu au kutofaulu kwa tasnifu. Aidha pia tutatazama nafasi ya mwandishi katika kulishughulisha suala la mwanamke.

Kwa jumla tasnifu hii imelishughulikia suala la mwanamke katika riwaya za Said Ahmed Mohamed. Tumechunguza jinzi mwandishi huyu alivyowasawiri wahusika wa kike katika kujenga maudhui ya kazi hizi.

Sura ya kwanza ni sawa na utangulizi ambao unatudokezea yale tutakayokumbana nayo katika tasnifu hii. Pia tatizo la utafiti limetatuliwa katika sehemu hii. Tumetaja madhumini ya tasnifu nadhania inayotumiwa kungoza tasnifu hii.Baada ya kuangalia sura ya kwanza ambayo ni sawa na mwongozo wa tasnifu tunaendelea maudhui ya riwaya ili kubainisha nafasi ya mwanamke katika jamii.

Katika misingi ya kifeministi, riwaya za mwandishi tulizozihakiki yaani *Asali Chungu*, Utengano, *Kiza Katika Nuru* na *Tata za Asumini* zinazotuonyesha mwamko wa wanawake kwa njia mbalimbali.

Kabla mwandishi hajatupeleka moja kwa moja hadi kwenye mwamko wa mwanamke, kwanza anatusawiria dhuluma mbali mbali ambazo mwanamke anazipitia katika jamii.

Dhuluma ambazo mwanamke anakumbana nazo ni pamoja na, dhuluma katika ndoa ambapo mwanamke anapoolewa hutumiwa kama mali ya mwanamume, na hivyo kukosa hali ya ubinadamu katika ndoa. Mara nyingi mwanamke hutazamwa kama kiumbe duni ambaye hana , mamlaka yeyote mbele ya mumewe. Wahusika ambao mwandishi ametumia katika kutimiza lengo hili ni pamoja na Amina wa *Asali Chungu*, Bi. Tamima na Mwanasururu wa *Utengano* na Bi. Kudura wa *Kiza Katika Nuru.*

Baada ya kuchunguza jinzi mwanamke alivyosawiriwa kama mdhulumiwa, tumechunguza pia juhudi mbali mbali anazozifanya mwanamke katika kutafuta ukombozi wake. Miongoni mwa malengo ya nadharia ya kifeministi ni kupigania kuwekwa wazi kwa juhudi zinazofanywa na wanawake katika kuinua hali zao katika jamii. Uhakiki wetu unalitimiza lengo hili kwa kuzimulika juhudi za wanawake wenzao na pia nafsi zao.

Wahusika tuliowaangazia kwa ujasiri wao wa kusimama imara na kudai haki zao na za wanawake wengine katika jamii ni pamoja na Bi. Pili wa *Asali Chungu* ambaye analalamika dhuluma za Bwana Zuberi dhidi ya Semeni miongoni mwa dhuluma zingine. Biti Kocho na Kazija wa riwaya ya *Utengano* pia ni mifano mizuri ya wanawake waliojitolea kukabiliana na wanaume huku wakipigania haki za wanawake.

Katika *Kiza Katika Nuru* Biti Jabu amesawiriwa kama mfano wa mwanamke anayoielewa jamii na kutambua madhila wanayoyapitia wanawake na hivyo kujitolea

katika kupigania kukomeshwa hujuma zozote kutoka kwa mwanamume dhidi ya mwanamke kupitia kwa Biti Jabu. Tunamwona Bi. Kudura akizinduka na kutambua jinsi alivyodhulumiwa kwa muda mrefu. Katika asasi ya ndoa na hivyo kuamua kukataa kunyanyaswa zaidi. Bi. Kudura anapinga hila za mumewe Bwana Juba ambaye anamtaliki.

Pia miongoni mwa malengo ya nadharia ya kifeministi ni kuzihakiki kazi za kifasihi ambazo zimeandikwa na wanaume kwa mtazamo wa kike. Lengo hili tumehitimiza kwa kuzihakiki riwaya za mwandishi Said Ahmed Mohamed ambaye ni mwanamume kwa kuzingatia mtazamo wa kike.

## 5.1 KUFANIKIWA NA KUTOFANIKIWA KWA MWANDISHI

Kwa kuzingatia mtazamo wa kifemnisti, tunaona kwamba kwa kiwango kikubwa, Said Ahmed Mohamed amefanikiwa. Katika usawiri wa wahusika wa kike katika harakati za kujitafutia uhuru wao kama tulivyoeleza hapo juu. Amefaulu katika suala hili kwa kuyaangazia matatizo yanayowakumba wanawake na hatimaye kuonyesha juhudi zao za kupigania uhuru wao.

Vile wahenga walivyosema, hakuna kizuri kisicho na kasoro, mwandishi huyo pia ana udhaifu wa kiwango fulani kutokana na vile amemsawiri mhusika wa kike udhaifu huu tutanangazia kumtia kwa jinsi alivyowasawiri wahusika, Amina na Semeni wa *Asali Chungu*, Maimuna na Mwanasururu wa *Utengano*, Rose wa *Kiza Katika Nuru* na

Asumini wa *Tata Za Asumini.* Mwandishi amewasawiri wahusika hawa kama mifano ya wale wanaodhulumiwa na wanaume na hivyo wanaojaribu kujinusuru kutokana na dhuluma hizo.

Wanapopata uhuru huo, wanashindwa kuudhibithi na mwishowe wanaishia kurudi mikononi mwa wanaume ili kunusurika.

## 5.2 KUHUSU NADHARIA TETE

Nadharia tete yetu ya kwanza ni kuhusu kujitokeza kwa suala la usawiri wa wahusika wa kike jambo ambalo limethibitika. Wahusika wa kike wamepewa nafasi katika riwaya hizi ili kuwasilisha mawazo mbalimbali kuwahusu wanawake katika jamii.Haya yamethibitika kulingana na maelezo ambayo tayari tumeyatoa hapo juu kama vile;mwanamke kisiasa, mwanamke kielimu, mwanamke kiuchumi na mwanamke katika ndoa.

Nadharia tete ya pili kuhusu kuyaangazia matatizo yanayokumba wanawake na juhudi wanazozifanya kujinusuru pia imethibitishwa na tayari tumeeleza hapo mbeleni kama vile matatizo ya kiuchumi, kisheria kisiasa na malezi ya mtoto wa kike.

Nadharia tete ya tatu kuhusu juhudi mbalimbali zinazofanywa na wanawake katika kutafuta ukombozi pia tumethibitisha kuwepo na kuonyesha udhaifu ulioko katika kumsawiri mwanamke akitafuta ukombozi. Wanawake mbalimbali wamesawiriwa wakiwa na mwamko wa kutetea maslahi yao na ya jamii kwa jumla.

## 5.3 MAPENDEKEZO KUHUSU UTAFITI ZAIDI

Said Ahmed Mohamed ameandika kazi za aina nyingi, riwaya ikiwa miongoni mwao. Tunapendekeza uhakiki wa kifeministi ufanyiwe kazi zingine za mwandishi huyu kama vile, hadithi fupi, tamthilia na hata ushairi.

Aidha tunapendekeza utafiti ufanywe ili kutambua nafasi ya uhakiki wa kifeministi katika fasihi ya Kiswahili.

Tatu tunapendekeza kubuniwa kwa nadharia mahususi itakayoongoza uhakiki wa masuala ya wanawake kwa vile bado nadharia ya kifemnisti ina utata mwingi.

# MAREJELEO


Abcarian, R, Klotz, M (1992) *Literature: The Humane Experience*, New York, St. Martin's Press, Inc.

Abrams, M.H (1981) *A Glossary of Literary Terms*, New York: Holt, Rine Hart and Winston.

Alamin, M, Syambo, B (1992) U*chambuzi Wa Fasihi*, Nairobi: East African Educational Publishers.

Beckson, K, Gunz, A (1960) *Literary Terms: A Dictionary*, New York: Farrah, Straus and Girohx Tuames

Boudon, R, Bourricaud, F (1982) *A Critical Dictionary of Sociology*, London: University of Chicago Press.

Chakita (2002) *Utafiti Wa Kiswahili*, Eldoret: Moi University Press.

Cuddon, J.A (1977) *A Dictionary of Literary Terms*, London: W & J Mackay Limited.

Davis, R, Finke, L (1989) *Literary Criticism and Theory*, New York: Long man Inc.

Davis, R, Schleifer, R (1989) *Contemporary Literary Criticism*, New York: Longman.

Egleton, M (ed. 1986) *Feminist Literary Theory: A Reader*, Oxford: Basil Blackwell Limited.

Fokkema , D. W , Elrud , K (1978) *Theory of Literature in The Twentieth Century* , London : C .Hurst & Co. (Publishers) Limited.

Franco, J (1989) *Plotting Woman*, London: Columbia University Press.

Home, C.T (1937) *The Single Parent Family, in Children's Books*, New York: The Scarecrow Press Inc.

Howthone, J (1984) *Criticism and Critical Theory, London*: Edward Arnold (Publishers) Ltd.

Khaemba, S.S (1999) *Ulinganishi Wa Maudhui ya Kimapinduzi Katilka Dunia Mti Mkavu na Kiza Katika Nuru*, Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa)

Kuthven, K.K (1984) *Feminist Literary Studies: An Introduction*, New York: Cambridge University Press.

Lerner, D.L (1954) *English Literature: An Interpretation for Students Abroad*, London : Oxford University Press.

Lughano, R (1989) *Usawiri Wa Wanawake Katika Riwaya Za Euphrase Kezilahabi*, Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Maggie, H (1996) *Feminist Literary Criticism in America and England*, In Women's Writing: *A Challenge To Theory*, Sussex: Harvesters Press.

Mbatiah, M (2001) *Kamusi ya Fasihi*, Nairobi: Standard Textbooks and Graphics and Publishing Ltd.

Mc Gann, J.J (Ed.1987) *Textual Criticism and Literary Interpretation, London*: The University of Chicago Press.

Mohamed S. A (1977) *Asali Chungu*, Nairobi: English Press Limited.

_____________ (1980) *Utengano*, Nairobi: Longhorn Publisher Ltd.

_____________ (1988) *Kiza Katika Nuru*: Nairobi: Oxford University Press.

_____________ (1990) *Tata Za Asumini*, Nairobi: Longhorn Publishers.

Montheith, M (Ed.1986) *Women's Writing: A challenge to Theory*, Sussex: Harvesters Press.

Njogu, K (1997) *Uhakiki Wa Riwaya Za Visiwani* Zanzibar, Nairobi: Nairobi University Press.

Njogu, K, Chimerah, R (1999) *Ufundishaji Wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Only, R (1981) *Aggressive Prose*, Dar es Salaam: Institute of Swahili Research.

Reeves, J (1956) *The Critical Sense: Practical Criticism of Prose and Poetry*, London: Heinemann Educational Books.

Rollins, J.D (1983) *A History of Swahili Prose*, Leiden: E.J Brill.

Scott, A.F (1965) *Current Literary Terms*; London: The Mc Millan Press Ltd.

Shreir, S(ed, 1988) *Women's Movements of The World: An International Directory and Reference*, London: Longman.

Susan, D (Ed. 1985) *The Complete Shorter Fiction of Virginia Woolf*, New York: Harcourt Brace Jovanovich, Publishers.

Susan, S.M.E (1989) *Policing Domestic Violence*, London: Sage Publications

TUKI, (1981) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research

_____, (1996) *English-Kiswahili Dictionary,* Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research

Tuttle, L (1986) *Encyclopedia of Feminism*, London: Longman Group Limited.

Wamitila, K.W (2002) *Unakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake,* Nairobi: Phoenix Publishers Limited..

EAST AFRICANA COLLECTION